


**SIMULIZI** aliyekaa miaka 36 jela kusubiri kitanzi
UKURASA 19

**WAWEKEZAJI** mbaroni tuhuma za kutorosha dhahabu kilo mbili
UKURASA 3



UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Juni 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580600

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# Ni mimi na ninyi

**SAMIA** aonya wateule wake, abainisha sababu kuteua ma-RAS wanawake...

*Endelea Uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan



## AJALI BASI ILIVYOKATA UHAI ABIRIA

UKURASA 2

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba (kushoto), akikagua basi la abiria la Kampuni ya Classic linalofanya safari zake kati ya Kampala, Uganda na Dar es Salaam, baada ya kupata ajali katika kona ya Didia, Kijiji cha Buyubi wilayani Shinyanga jana na kuua watu wanne, 20 kujeruhiwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Majaji 3, mawakili 15 kesi vigogo CHADEMA

UKURASA 7

**MICHEZO** **WABONGO WAMPONZA SAMATTA KUREJEA VILLA** UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**



Viongozi mbalimbali walioapishwa pamoja na kuteuliwa katika nafasi tofauti wakila kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma, baada ya kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Ajali ilivyokata uhai wa abiria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine 20 kujeruhiwa katika ajali ya basi ya Kampuni ya Classic, likitokea Kampala nchini Uganda kwenda jijini Dar es Salaam.

Ajali hiyo ilitokea majira ya saa 10 alfajiri kuamkia jana katika kona ya Didia, wilayani Shinyanga na kusababisha vifo vya abiria wanne na majeruhi 20 huku wengine wakikatika viungo vya mwili.

Mmoja wa abiria aliyekuwa kwenye basi hilo, Fotuna Wilbert, alisema baada ya kufika kwenye kona hiyo basi likiwa katika mwendo kasi, waliona basi hilo likiyumba na kumshinda dereva na kupata ajali.

Maimuna Mohamed, alisema alikuwa amelala na aliposikia kishindo kikubwa alishtuka na kukuta tayari wamepata ajali, huku wenzake wakiwa wameumia na kukimbizwa hospitalini.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwataja waliofariki kuwa ni Wahida Yusuph, Joseph Joseph, Rehema Haji na Nasorro Hamisi.

Aliwataja majeruhi watano waliokatika viungo kuwa ni Njama Hassani, Fatuma Kesi, Sada Manga na Twalibu, ambao wamekatika mkono wa kushoto na mmoja mguu wa kulia, pamoja na Mohamed Daudi mkono wa kulia.

Alisema majeruhi wengine 15 walitibiwa na kuruhusiwa na hali zao zinaendelea vizuri.

Kamanda alisema basi hilo lilikiwa na abiria 43.

"Chanzo cha ajali hii ni mwendo kasi, dereva wa basi anayejulikana kwa jina la Maxison Mkuru, alishindwa kukata kona na kusababisha ajali, na tunamsaka sababu amekimbia," alisema Magiligimba.

Pia alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga na majeruhi wanaendelea na matibabu, aliwaonya madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani.

# Samia: Ni mimi na ninyi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema hatawavumilia viongozi wa mikoa wakiwamo makatibu wakuu wa mikoa na wakuu wa mikoa watakaoshiriki na kuwa vyanzo vya migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao.

Amewataka kwenda kutekeleza majukumu yao kwa bidii kwenye ofisi za umma, akisema hatakuwa tayari kuuvumilia utendaji duni.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma katika hafla ya kuwaapisha makatibu wakuu wa mikoa 11 aliowateua pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu (Kazi Maalum), George Mkuchika.

Alisema makatibu tawala wa mikoa ni wasimamizi na washauri wa wakuu wa mikoa na kwamba kukua kwa uchumi katika maeneo hayo kunategemea ushauri wao kwa watendaji wote wa mikoa.

"Usimamizi wa watumishi katika mikoa unawategemea ninyi ma-RAS. Sitavumilia RAS, mkuu wa mkoa kujiingiza katika migogoro ya wakulima kwenye maeneo yao.

"Ninyi ni wasimamizi wa shughuli zote za mikoa, mna kazi kubwa, watumishi wote wako chini yenu.

"Majukumu yaliyo mbele yenu ni makubwa mno, mnakwenda kuwa makatibu wa tawala wa mikoa, kamati za usalama, sekretarieti na watendaji mikoa na wilaya, wakuu wa utumishi na maofisa masuhuli. Tukisema asilimia 40 ya mapato, iende kwenye maendeleo haikwenda ni ninyi," alisema.

Alisema utendaji mzuri kwenye mikoa unatokana na wao, hivyo usimamizi kutoka ngazi ya chini ya uongozi kutoka serikali za mitaa hadi serikali kuu.

Rais Samia alisema anatarajia ubunifu mkubwa kutoka kwa ma-RAS hao na kusisitiza kwenda kusimamia uchumi katika maeneo yao, hususan kwenye viwanda na uwekezaji.

"Kila niliyemteua ajue kuna mtu anamfuata nyuma yake na hamjui. Mikoani kuna uzembe, upendeleo mkubwa kwa watumishi. Kuna wakati DC (Mkuu wa Wilaya) mkoa fulani alijimilikisha maeneo, DC kama huyu unamwacha wa nini?" Rais Samia alihoji.

Ninyi ndiyo jicho langu, ujuzi wa kufahamu kuna mabati mangapi sehemu fulani sina, alikuwa nao Hayati John Magufuli, mimi ujuzi wangu kwenye uchumi. Wakuu wa mikoa ndio jicho langu.

"Migogoro ya mirathi, wanawake ndiyo wanalia zaidi, migogoro ya ardhi, bado ipo nendeni mkasimamie, sitavumilia kusikia RAS, RC, mkajiingiza kwenye mkoa, anakuta kuna ardhi ya watu anajimilikisha, mmepelekwa kwa kazi maalum," alionya.

Rais Samia aliagiza makatibu hao wakasimamie utumishi wa umma na kufuatilia watumishi ambao hawafiki kazini na kisha mafaili yanapomfikia, hukana rufani.

"Utakuta mtumishi hayupo kazini wiki mbili, halafu baadaye anakata rufani kwamba 'mimi nilikuwa kazini', makatibu mpo, wakuu wa mikoa mpo, msimamie hili, mimi na ninyi," alionya.

Alisema wajibu wa viongozi hao ni pamoja na kuhakikisha mazingira yanatunzwa kwenye maeneo yao, ili kuhakikisha vizazi vijavyo vinarithi mazingira mazuri.

Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango aliwataka viongozi hao kwenda kutatua migogoro ya ardhi.

"Kero bado ni nyingi za wananchi, Mkoa wa Morogoro ni kati ya maeneo ambayo napokea barua nyingi kuhusu migogoro ya ardhi," alisema Dk. Mpango.

Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, alisema makatibu hao wana majukumu makubwa katika kusimamia serikali na utendaji kwenye mikoa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema anatarajia viongozi hao walioteuliwa hawatamwangusha Rais.

Mwalimu alisema iwapo utendaji kazi wa makatibu tawala hao utakuwa imara, watafanikiwa kuongeza makusanyo hadi Sh. trilioni moja kutoka Sh. bilioni 840 kwa mwaka katika halmashauri 184 nchini.

# ...ataja kiini kuteua ma-RAS wanawake

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema asilimia 46 ya viongozi wanawake walioteuliwa kuwa makatibu tawala (ma-RAS) imetokana na kutambua uwezo wao kwenye wadhifa huo.

Amesema kuongezeka kwa idadi hiyo ni mtihani kwa viongozi wanawake ili kuleta tofauti ya utendaji, ikizingatiwa nafasi hizo awali ziliongozwa zaidi na wanaume. Rais Samia aliyasema hayo jana Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma katika hafla ya kuwaapisha Ma-RAS 11 aliowateua pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu, George Mkuchika, iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, mawaziri na wakuu wa mikoa. "Utendaji wa wanawake hususan katika uadilifu na uaminifu unafahamika kulinganishwa na ma-RAS wanaume, ambao kwa asilimia kubwa ndiyo walioshika nafasi hizi hapo awali.

"Nimefanya hivi nikijua wanawake mna uwezo mkubwa wa kwenda kufanya kazi hii, hamna sababu ya kwenda kuwa wanyonge, nimeweka asilimia 46 makusudi. "Mnatakiwa kuwa waadilifu, uaminifu na unyenyekevu kwa watu, wananchi wa kawaida, si kwa mabosi wetu, wanawake mnaiweza kazi hii vizuri. Huu ni mtihani kwenu tofauti na ilipokuwa ma-RAS wengi wanaume, tuone mabadiliko," alifafanua. Rais Samia alisema hatua ya kuongeza idadi ya wanawake viongozi katika nafasi mbalimbali inaleta uwiano wa uongozi.

"Ile mikoa ambayo kuna wanawake kwa wanawake, sijui itakuwaje, lakini tunawaangalia ili vipi usibababishe nisije nikaisikia, pale ninyi si wanawake, ni Mkuu wa Mkoa na RAS wake.

"Mkienda kufanya hivyo mnanitia aibu, yatakayosemwa ndiyo shughuli ya wanawake. Kwa nini msikae pamoja? Mbona mnaolewa wawili mnakaa pamoja? Kwanini katika kazi? Mkachape kazi, hiyo mikoa ninaitegemea sana," aliagiza.

Alisema anatarajia mikoa iliyo na viongozi wengi wanawake itafanya kazi nzuri kama ilivyo mikoa mingine inayoongozwa na wanaume na kwamba Tanzania itachangiwa na jinsi yeyote na imani yoyote katika kuliletea taifa maendeleo.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, akionyesha dhahabu zilizokuwa zimefichwa ili kutoroshwa na kukwepa kodi, na mwekezaji wa Kitanzania kwa kushirikiana na raia wawili wa China, huko Ulanga, mkoani Morogoro jana. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Tanzania kuzalisha MW 5,000 za umeme

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Nishati imebainisha vipaumbele vyake, ikijipanga kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kwa miaka mitano ijayo inayolenga kuzalisha megawati 5,000 za umeme.

Waziri wake, Dk. Medard Kalemani, alibainisha hayo bungeni jijini Dodoma jana alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/22.

Kwa mwaka ujao wa fedha, wizara hiyo inatarajia kutumia Sh. trilioni 2.386 kukiwa na ongezeko la asilimia nne kulinganishwa na Sh. trilioni 2.197 zilizotengwa kwa ajili ya mwaka 2020/21.

Dk. Kalemani alisema kuwa katika mwaka ujao wa fedha, watatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ukiwamo wa Bwawa la Julius Nyerere (megawati 2,115), Ruhudji (megawati 358) na Rumakali (megawati 222).

Miradi mingine ni Kinyerezi I -Extension (megawati 185), Rusumo (megawati 80), Malagarasi (megawati 49), Mtwara (megawati 300) na Somanga Fungu (megawati 330).

Waziri Kalemani alisema pamoja na miradi hiyo ya uzalishaji umeme, serikali pia itaendelea kuimarisha mifumo ya usafirishaji umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ukiwamo mradi wa kusafirisha umeme wa: North -West Grid Extension kV 400; Singida -Arusha -Namanga kV 400; na Rufiji -Chalinze -Dodoma kV 400.

Mingine ni Chalinze -Kinyerezi kV 400; Rusumo -Nyakanazi kV 220; Geita -Nyakanazi kV220; Ibadakuli (Shinyanga) -Imalilo (Simiyu) kV 220; Tabora-Kigoma kV 132; Tabora-Katavi kV 132; pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Handeni na Kilindi mkoani Tanga.

Waziri Kalemani alitaja maeneo mengine ya kipaumbele yatakayozingatiwa na wizara ni kuendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu mzunguko wa pili wa mradi kabambe wa kupeleka umeme vijijini.

Pia alisema wataendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (EACOP) kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga; mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG); na Utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitaluvya kimkakati vikiwamo Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi Wembere.

Alisema wamejipanga kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji wa taasisi zilizopo chini ya wizara (TANESCO, TGDC, REA, TPDC, PURA na PBPA) ili kuongeza ufanisi katika sekta hiyo.

Waziri huyo alisema wizara pia itazingatia kuwajengea uwezo watumishi wake na taasisi zake katika kusimamia sekta kwa kuboresha mazingira ya kazi ili kutoa huduma bora na kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya nishati.

**HALI YA UMEME**

Waziri Kalemani alisema hali ya upatikanaji wa umeme nchini imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Aprili mwaka huu, jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika gridi ya taifa ilifikia megawati 1,573.65.

Kati yake, megawati 573.7 zinatokana na vyanzo vya maji, megawati 901.32 gesi asilia na megawati 10.50 tungamotaka (Biomass).

Alisema uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia asilimia 86.57 na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPP/SPPs) ambayo huchangia asilimia 13.43.

"TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa gridi ya taifa yenye uwezo wa kuzalisha megawati 32.21 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia megawati 1,605.86," alisema.

**MAHITAJI UMEME**

Waziri Kalemali alisema mahitaji ya juu ya umeme nchini yameendelea kuongezeka na kufikia megawati 1,183.28, sawa na ongezeko la asilimia 2.75 kulinganishwa na megawati 1,151.66 ya mwaka 2019/20.

"Hadi kufikia Machi mwaka 2021 jumla ya urefu wa njia za kusafirisha umeme umefikia kilomita 6,111.27 sawa na ongezeko la asilima 25.94 kulinganishwa na kilomita 4,852.7 za mwaka 2015/16.

"Kati ya hizo, njia za msongo wa kV 400 ni kilomita 670; kV 220 ni kilomita 3,225.7; kV 132 ni kilomita 1,672.57; na kV 66 ni kilomita 543," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu, miundombinu ya usambazaji umeme iliendelea kuongezeka na kufikia jumla ya kilomita 147,156.8, sawa na ongezeko la asilimia 139.77 kulinganishwa na kilomita 61,373.76 zilizokuwa zimefikiwa Juni 2015.

Alisema kati yake, njia za msongo wa kV 33 ni kilomita 47,106.07, msongo wa kV 11 ni kilomita 12,457.21 na msongo wa kV 0.4 ni kilomita 87,593.52.

# Wawekezaji mbaroni tuhuma kutorosha dhahabu kilo mbili

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MWEKEZAJI mzawa, Junior Kasanga na raia wawili wa China, wamekamatwa wilayani Ulanga, wakijaribu kutorosha madini ya dhahabu kilo mbili, yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 337.5 yaliyochimbwa Kijiji cha Isyanga, wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya kwa kushirikiana na kamati yake ya usalama ya wilaya, alisema waliwakamata wawekezaji hao wakitorosha madini kiasi cha gramu 2,460.

"Ulanga inafahamika kwa madini na ndani ya wilaya tumekaribisha wawekezaji, wachimbaji wadogo na wakubwa, lakini katika shughuli za uchimbaji, tunaendelea kuwasihi wachimbaji kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za nchi kulingana na sekta yao ya madini," alisisitiza.

Alisema wachimbaji wanapopata madini ni lazima kuyafikisha kwanza kwenye ofisi za madini kwa ajili ya uhakiki na baadaye taratibu zaidi zifuatwe.

"Sisi kama serikali tuko macho, hatuwezi kuruhusu ubadhirifu wa aina hii, hizi ni mali za Watanzania, mnapopewa leseni muwe waaminifu," alisema Ngolo.

Aliwataka wafanyabiashara na wawekezaji wengine kuwa waaminifu kwa kulipa kodi na kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi. Aliwaonya wengine wenye kutaka kutumia Ulanga kama kichochoro cha kukwepa kodi na kufanya biashara kwa njia ya magendo, wakibainika watachukuliwa hatua kali za kisheria na tayari watuhumiwa hao wako mikononi mwa polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

Kaimu Ofisa Migodi Mahenge, Edward Lubinja, alisema mtuhumiwa Kasanga siku moja kabla ya kukamatwa, alifika katika ofisi za madini akiwa na gramu 524 kwa ajili ya kuthaminishwa, lakini waliingia shaka na kiwango hicho na kuamua kufanya ufuatiliaji wa siri na kubaini kuwa alikuwa na mzigo zaidi aliopanga kuutorosha. "Baada ya kumfanyia upekuzi, ndio tukabaini alikuwa na mzigo mwingine wa madini wenye gramu 2,460, wa thamani inayokadiriwa kufikia Sh. 337,500,000, tumewafikisha polisi kwa ajili ya taratibu zaidi za kisheria, kwani walikuwa wanakwepa kulipa kodi halali ya serikali," alisema Lubinja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim, alipoulizwa, alikiri kukamatwa kwa watuhumiwa wanne kwa tukio hilo na walikamatwa maeneo ya Lupiro, katika barabara kuu ya Ulanga-Ifakara.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni Mohamed Musa ambaye ni dereva, Junior Money Kasanga ambaye ni miliki wa mgodi na raia wawili wa China, You Wu na Weg Hua.


KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

DAR ES SALAAM

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

MIRATHI NA 23 YA MWAKA 2021

MAOMBI YA BARUA USIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU

**MARK DANHI BOMANI**

MWOMBAJI/WAOMBAJI

**RAHMA BOMANI NA HERI MARK BOMANI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji/waombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 17th mwezi wa JUNE 2021

Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe **5th mwezi wa MAY 2016.**

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI

## Ajira 1,900 zaja

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Nishati imesema katika mwaka wa fedha 2021/22 inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 1,925 katika taasisi zilizo chini yake.

Waziri wake, Dk. Medard Kalemani. aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/22.

Alisema kati ya ajira hizo, Shirika la Umeme (TANESCO) litapata watumishi wapya 1,856, Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC) 34, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) 15 na Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Mafuta (PURA) 20.

Waziri huyo alisema wizara inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 70, kuwathibitisha kazini watumishi 14 na kumbadilisha kada mtumishi mmoja.

Alisema wizara katika mwaka wa fedha 2020/21 iliwajengea uwezo watumishi wawili katika mafunzo ya muda mrefu na 260 katika mafunzo ya muda mfupi.

Alisema kwa mwaka 2021/22, wizara inatarajia kupeleka mafunzo ya muda mrefu watumishi saba na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 52.



Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu (wapili kushoto) na wenzake wawili wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza wakati wakiingia kwenye chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza mashtaka ya uhujumu uchumi yanayowakabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kesi aliyekuwa Mkurugenzi NIDA kusikilizwa mfululizo

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya Uhujumu Uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Nickson Maimu na wenzake wanne inatarajia kuendelea kusikilizwa mfululizo Juni 16 na 17, mwaka huu.

Aliyekuwa Ofisa Utumishi NIDA, Rehema Ndahami, alitoa ushahidi wake jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Rehema alidai aliajiriwa mwaka 2011 akamkuta Maimu NIDA na ndipo alipomfahamu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Zacharia Ndaskoi, alidai kwamba alipewa maelekezo ya kupeleka baadhi ya nyaraka za washtakiwa TAKUKURU na nyaraka hizo ni barua za uteuzi ikiwamo ya Maimu iliyokuwa ikionyesha kateuliwa kushika nafasi aliyokuwa nayo Desemba 2009.

Pia alipeleka barua ya mshtakiwa, Sabina Raymond, aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Masuala la Sheria NIDA na barua ya uhamisho ya mshtakiwa, George Tarimo, aliyekuwa Ofisa Usafirishaji.

Akiongozwa na Wakili Ndaskoi, alidai uamuzi unaofanywa na kiongozi mkuu ni kwa manufaa ya taasisi na serikali.

Alidai kiongozi mkuu kabla ya kufikia uamuzi anatakiwa kufuata taratibu na mwongozo, asipofanya hivyo kikitokea kitu atawajibika.

Shahidi alidai mshtakiwa anapotuhumiwa hukabidhi ofisi kwa ajili ya kupisha uchunguzi, lakini washtakiwa katika kesi hiyo walipotuhumiwa walisimamishwa kazi bila kukabidhi ofisi.

Shahidi alimaliza kutoa ushahidi na hapakuwa na maswali kwa upande wa utetezi, kesi iliahirishwa hadi Juni 16 na 17 mwaka huu, kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Maimu, Meneja Biashara, Aveline Momburi, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

Washtakiwa wanakabiliwa na jumla ya mashtaka 55 yakiwamo ya kusababisha hasara ya Sh. bilioni 1.175, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa mwajiri na matumizi mabaya ya madaraka.

Wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari 15 hadi 19 mwaka 2010 katika Makao Makuu ya NIDA Kinondoni.

# Mwinyi: Nilifichwa taarifa za mauaji ya waganga

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema mauaji ya vikongwe yaliyochagizwa na imani za kishirikina kwenye mikoa ya Mwanza na Shinyanga ni miongoni mwa sababu zilizomsukuma kujiuzulu.

Amesema kuwa kwa uchungu mkubwa, akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliamua kuandika barua ya kujiuzulu ili kulinda heshima yake na kwa serikali iliyokuwa ikiongozwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mwinyi anasimulia hayo kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', akisema Januari 22 mwaka 1977 alimwandikia barua Mwalimu Nyerere iliyojenga hoja ya sababu za kujiuzulu.

"Waziri Mkuu, Rashidi Kawawa akaitisha kikao Januari 24 mwaka 1976, kujadili kadhia hiyo na kukomesha mauaji hayo.

"Nilikuwapo mimi na wadhifa wangu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi... ikaamuliwa ianzishwe operesheni maalum. 'Operesheni Mauaji' kwa lengo la kuwakamata na kuwahoji watuhumiwa.

"Ni dhahiri tuliyokuwa tunapambana nayo yalihusu mambo ya kishirikina, ni dhahiri walengwa wakuu wangekuwa waganga wa kienyeji," anasema.

Mwinyi anasema kuwa wakati wa mahojiano ya kubaini kinachosababisha, baadhi walivuka mipaka ya utaratibu, kuzingatia utaratibu wa kuhoji na kusababisha watuhumiwa wengine kuuawa.

"Nilifichwa, sikujua mpaka Mwalimu Nyerere akawa amepata taarifa na kuunda tume ya uchunguzi. Nikajihisi ninao wajibu wa kujiuzulu ili kulinda heshima ya serikali na kiongozi wake; Mwalimu Kambarage Nyerere," anasema.

Mwinyi anasema kujiuzulu kwake kulikuwa hiari na siyo shinikizo kutoka kokote na kwamba Waziri mwenzake, Peter Siyovelwa na wakuu wa mikoa ya Mwanza na Shinyanga walilazimika kuchukua hatua.

"Bado ninaamini uamuzi wangu ulikuwa sahihi na nadhani ulinijengea heshima serikalini na kwenye jamii kiasi fulani," anasema.

Katika sehemu ya barua ya kujiuzulu kwake aliyoiambatanisha kwenye kitabu, Mwinyi anasema;

"Kwa hiyo, Mwalimu ninakuomba mambo matatu. Kwanza, ninaomba radhi mimi nafsi yangu na pia ninaomba radhi kwa niaba ya askari wote walio wema.

"Pili, ninaomba vilevile uelewe sehemu yangu katika kosa hili. Tatu, kwa fedheha hili, ninaomba unikubalie nijiuzulu."

HABARI KITAIFA

# Vigogo wa TRA wapiga kambi siku saba Kigoma

**Na Mwandishi Wetu,**
KASULU

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Alphayo Kidata, amepiga kambi ya wiki moja mkoani Kigoma kwa lengo la kutoa elimu kwa walipakodi mlango kwa mlango.

Kigogo huyo wa TRA amefuatana na viongozi wengine wa mamlaka hiyo wakiwamo Kamishna wa Kodi za Ndani, Hebert Kabyemela, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, na Naibu Kamishna wa Walipakodi Wakubwa, Beatus Nchota.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (kulia), akizungumza na watumishi wa mamlaka hiyo mkoani Kigoma juzi, wakati akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo. **PICHA: TRA**

Kamishna Kidata amekwenda na timu ya wataalamu kutoa elimu na huduma kwa mlipakodi kwa lengo la kutatua kero zilizojitokeza mkoani humo na kuhakikisha wanapita kila duka, yaani mlango kwa mlango kuwaelimisha wafanyabiashara kuhusu sheria na taratibu za ulipaji kodi.

Akizungumza na viongozi wa wafanyabiashara katika Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma, Kamishna Mkuu Kidata alisema timu hiyo ya wataalamu wa elimu kwa mlipakodi watakaa wilayani humo kwa wiki nzima wakipita duka kwa duka kutoa elimu ya kodi na kutatua haraka kero za kikodi zinazowakabili wafanyabiashara hususani makadirio ya kodi.

"Ndugu zangu nimepokea maoni, ushauri na changamoto zenu na mimi kwa kulitambua hili nimekuja na timu ya wataalamu kutoka TRA Makao Makuu ambao nitawaacha hapa kwa ajili ya kuwaelimisha sheria na taratibu za ulipaji kodi ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wenu.

"Pia, watamsikiliza kila mfanyabiashara mwenye changamoto na kuzitatua," Kamishna Kidata alisema.

Aliwaambia viongozi hao kwamba ni muhimu kila upande, yaani wafanyabiashara na watumishi wa TRA kuzingatia haki na wajibu wao kila wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

"Sisi watumishi wa TRA tunafanya kazi kwa kufuata misingi yetu ya maadili ambayo ni uwajibikaji, uadilifu na weledi, lakini kama mmoja wenu alivyosema, ni lazima pia sote, ninyi na sisi TRA tuzingatie haki na wajibu kila tunapotekeleza majukumu yetu," alisema.

Viongozi hao walisema wamefurahishwa na kitendo cha Kamishna Mkuu wa TRA kufika wilayani huko na kufanya nao mazungumzo na kupeleka timu ya wataalamu kutoa elimu kwa walipakodi hao kwa lengo la kutatua kero zilizojitokeza baina ya wafanyabiashara wa wilayani Kasulu na watumishi wa TRA.

"Ndugu Kamishna Mkuu tunakushukuru sana kwa kuja kuzungumza na sisi na tumefurahi sana kwa kutuletea watalaamu wa kutuelimisha na kutatua kero mfanyabiashara mmoja mmoja kama zilivyowasilishwa kwako leo," alisema Prosper Guga, Katibu wa Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) wilayani Kasulu.

Kabla ya kuzungumza na viongozi hao wa wafanyabiashara wa Kasulu, Kamishna Mkuu Kidata alipata nafasi ya kuwatembelea baadhi ya viongozi wa serikali mkoani Kigoma ambapo alifanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Anga, na Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Simon Anange.

Kamishna Mkuu pia alipata fursa ya kuzungumza na watumishi wa TRA wa Mkoa wa Kigoma na kuwataka kuzingatia kufanya kazi kwa bidii na weledi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati na hiari huku waki wapatia elimu ya kodi.

Hivi karibuni, wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma walifanya mgomo wa kufunga maduka wakidai kuwa watumishi wa TRA wilayani humo hawana lugha nzuri na wanawakadiria makadirio makubwa, suala linalowapelekea kushindwa kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, kutokana na mazungumzo yaliyofanyika baina ya viongozi mbalimbali wa serikali na wafanyabiashara hao, tayari maduka yamefunguliwa na shughuli za kibiashara zinaendelea kama kawaida.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chato kuwa mkoa iachiwe mamlaka

**MJADALA** unaoendelea sehemu mbalimbali nchini kuhusu uhalali wa Chato kuwa mkoa unazidi kushamiri katika mitandao ya kijamii, kila mtu akitoa maoni yake kuhusu uhalali huo, huku baadhi wakiunga mkono na wengine wakipinga.

Pia kumekuwapo na maandiko mbalimbali kutoka kwa baadhi ya viongozi wa dini pamoja na wadau yanayopinga mchakato huo.

Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya mwaka 2012, idadi ya wakazi wa Wilaya ya Chato ilihesabiwa kuwa 365,127.

Chato ilianzishwa mwaka 2007 kutokana na maeneo ya Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera, mwaka 2012 ikasogezwa katika mkoa mpya wa Geita.

Mwanzoni mwa Machi, mwaka huu, kulifanyika kikao maalum cha ushauri cha Mkoa wa Geita na kuridhia kuanzishwa kwa mkoa mpya wa Chato na kupendekeza mkoa huo mpya kuwa na wilaya tano, huku mkoa mama wa Geita ukibaki na wilaya tatu.

Kikao hicho pia kiliridhia Hifadhi ya Taifa ya Rubondo, kutoka Geita na kwenda mkoa mpya wa Chato, lakini Baraza la Madiwani mkoani Chato lilipinga hatua hiyo na kusababisha kuwapo kwa mvutano baina ya pande hizo mbili.

Baada ya makubaliano ya pamoja Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemery Senyamile, akatangaza kuwa mkoa mpya wa Chato utaundwa na wilaya tano ambazo ni Chato, Bukombe, Ngara, Biharamulo na Kakonko huku Mkoa wa Geita ukibaki na wilaya za Geita, Mbogwe, Busanda na Nyangwale.

Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akihutubia katika mazishi ya Hayati John Magufuli, aliagiza mamlaka husika mkoani Geita kuharakisha mchakato huo na kupeleka serikalini ili kuangaliwa kama Chato imekidhi vigezo vya kuwa mkoa au la.

Hata hivyo, baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakipinga mchakato huo wa Chato kuwa mkoa wakidai kwamba haujakidhi vigezo.

Ni vyema suala hilo likaachiwa mamlaka husika kulishughulikia na kulitolea uamuzi kuliko hiki kinachofanyika sasa, kuleta malumbano ambayo hayana afya kwa taifa.

Kuna taratibu za uanzishaji wa mkoa mpya ambazo serikali iliziweka na inazifahamu, hivyo ni imani kwamba zitafuatwa ili kukamilisha utaratibu huo badala ya kuwapo malumbano ambayo hayajengi.

Mchakato wa Chato kuwa mkoa ulianzishwa na Hayati Magufuli ambaye alikuwa na malengo na maono yake, lakini kuondoka kwake kusiwe chanzo cha mfarakano ya mchakatao huo ambao unaweza kuangaliwa upya na kupata mwelekeo mzuri.


Watanzania wanapaswa kuwa na subira kuhusu mapendekezo ya kuanzishwa kwa mkoa huo kwa sababu suala hilo liko katika hatua za awali.

Ni vyema Watanzania wakaacha kuhamaki katika mjadala huo kwa kuwa mapendekezo ya kikao maalumu cha ushauri (RCC) Mkoa wa Geita kuhusu suala hilo lazima yapitie mchakato mrefu kuamuliwa kwa mujibu wa vigezo, masharti na mahitaji.

Kuna mikoa mingi ilianzishwa kama vile Njombe, Katavi, Geita, Songwe na hakukuwapo na msuguano wowote wa kisiasa wala kijamii.

Hakuna haja ya majibizano wala malumbano, iachiwe mamlaka kufuata taratibu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuwe makini kufanikisha kukwepa yanayokaribisha magonjwa mlipuko

Na Sabato Kasika

**MTINDO** wa baadhi ya watu wa kutozingatia usafi wa mazingira, hutajwa kuwa miongoni mwa vyanzo vinavyosababisha kuenea maradhi na kuhatarisha afya za wahusika na wengine.

Utupaji taka ovyo kama kinyesi, majitaka na nyingine, vinaweza kusababisha matatizo ya afya, hivyo suala la kuzingatia usafi wa mazingira ni muhimu ili kuepusha watu kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

Hivyo, wale ambao wamezoea kuchafua au kutozingatia usafi wa mazingira, ni vyema wakatambua kuwa wana nafasi kubwa ya kuhatarisha afya zao na za wengine wanaowazunguka.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Afya Duniani (WHO), limekuwa likihimiza usafi wa mazingira, kwa kuwa uboreshaji wa mazingira una manufaa makubwa katika jamii hasa kuepusha mlipuko wa magonjwa.

Usafi wa mazingira ni muhimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa afya inazingatiwa kila sehemu, iwe nyumbani au kwenye shughuli mbalimbali ili kuzuia uwezekano wa binadamu kukabiliana na athari za taka.

Hata hivyo, baadhi ya watu hasa kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam, hutiririsha majitaka kutoka katika vyoo vyao kwenda mitaani mvua inaponyesha na kuibua harufu kali inayohatarisha afya zao na za wengine.

Wapo wanaofanya hivyo kwa madai kwamba, hawana uwezo wa kulipia magari ya kunyonya majitaka na kutokana na hilo, wengine hujenga vyoo kando ya mito na kuelekeza humo mabomba kutoka vyooni.

Mtindo huo kwenye baadhi ya maeneo umekuwa kama wa kawaida, ambapo wengine wakivizia hadi usiku wa manane na kutiririsha majitaka hayo, hali ambayo kimsingi ni uchafuzi wa mazingira na ni hatari kiafya.

Itakuwa vyema, iwapo mamlaka husika zitafuatilia hali hii na kuipatia ufumbuzi wa kudumu ili kulinda afya watu kuliko kundi dogo kuendelea kuhatarisha afya za wengine kwa kuchafua mazingira.

Kwa mfano, baadhi ya mabomba ya maji ya kunywa huku mingine ikiwa imechakaa na kufungwa mipira, imepitishwa kwenye mitaro ambayo wapo watu wamegeuza kuwa sehemu ya kutiririshia majitaka yao.

Ni wazi kwamba, hali kama hiyo ni rahisi majitaka kuingia ndani ya mabomba hayo na kuchanganyika na maji ya kunywa, na hivyo inakuwa ni rahisi watu kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kama watayatumia.

Ikumbukwe kuwa, pamoja na kuwapo kwa elimu inayohusu unywaji maji yaliyochemshwa, bado wapo baadhi ya watu wasiochemsha, hivyo katika mazingira hayo ni rahisi wao kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Kimsingi, jamii inapaswa kutambua kuwa, uboreshaji wa mazingira una manufaa makubwa kiafya, hivyo mmoja wetu kwa nafasi ahakikishe anasafisha mazingira yanayomzunguka.

Usafi uwe ni pamoja na kuacha kutiririsha majitaka ovyo, kutojisaidia ovyo na pia kufanyia biashara katika mazingira safi ili kuepuka kukumbwa na magonjwa ya mlipuko ambayo huibuka mara kwa mara.

Katika maisha, kila siku wapo baadhi ya watu wasiozingatia usafi wa mazingira kwa kufanya biashara ama shughuli zao kwenye mazingira machafu bila kujali kuwa ni hatari kwao na kwa wateja wao.

Imekuwa kama jambo la kawaida kukuta baadhi ya mama lishe na baba lishe kufanyia biashara zao katika mazingira machafu, hali ambayo si salama kwao na kwa wateja wanaofika kupata huduma ya chakula.

Njia mojawapo ya kupunguza, kama si kumaliza mtindo wa kutozingatia usafi wa mazingira ni kuendelea kuwapo kwa elimu kwa wahusika ili kila mmoja atambue umuhimu wa kuwa katika mazingira safi.

Kila kukicha wamekuwa wakiibuka watu wapya hasa kwenye biashara ikiwamo ya mama lishe na baba lishe, hao wote wanatakiwa kuelimishwa kuhusu usafi wa mazingira ili walinde afya zao na wateja wao. Elimu ikitolewa ipasavyo, wahusika wakaielewa na kuizingatia, ninaamini hakutakuwa na utiririshaji wa majitaka mitaani au kwenye mito ama mama lishe na baba lishe kuandalia vyakula katika mazingira machafu.

Kwa ujumla ni kwamba, elimu ya afya iendelee kutolewa kwa kina huku wale ambao watakuwa wanakiuka, wabanwe na sheria ndogondogo za halmashauri, kwani afya bora ni mtaji mkubwa.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yawahoji udanganyifu mabilioni

**Na Kulwa Mzee**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewahoji kwa mara nyingine watuhumiwa watatu kati ya sita wanaodaiwa kujipatia zaidi ya shilingi bilioni nne kwa kuidanganya Benki ya NBC.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kudanganya kwamba wafanyakazi 78 wa Kampuni ya Peertech ni wafanyakazi wa kudumu na kampuni hiyo imewadhamini wapewe mkopo wa Sh. 4,786,800,000 na Benki ya NBC wakati ni uongo.

Wakili wa Serikali kutoka TAKUKURU, Dickson Shayo, jana aliiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele, wapewe watuhumiwa watatu waliopo Gereza la Segerea kwa ajili ya mahojiano.

Washtakiwa walioombwa ni Baraka Madafu, Lusekelo Mbwele na Leena Joseph na mahakama ilikubali kuwapa watuhumiwa hao.

"Mahakama inakubali maombi, ni maombi ya kawaida lakini watuhumiwa mmewachukua wakiwa salama hivyo muwarudishe wakiwa salama," alisema Hakimu Kassian.

Watuhumiwa wengine katika kesi hiyo ni Mark Mposo, Benard Mndolwa na Silvina Karugaba ambao wanatuhumiwa kwa mashtaka 11 yakiwamo ya kughushi manne, kuwasilisha nyaraka za uongo manne, kujihusisha na genge la uhalifu, kujipatia kiasi hicho cha fedha kwa udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 4.78.

Inadaiwa kati ya Desemba 4, mwaka 2018 na Desemba 3, mwaka 2020 katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, walijihusisha na genge la uhalifu na kujipatia Sh. 4,786,800,000 kwa udanganyifu.

Katika shtaka la pili inadaiwa katika kipindi hicho walighushi mkataba wa udhamini wa mkopo wakionyesha kwamba watumishi 60 ni waajiriwa wa Kampuni ya Peertech na wana mikataba ya kudumu hivyo kampuni inawadhamini kupata mkopo.

Shtaka la tatu waliwasilisha nyaraka hiyo Benki ya NBC Masaki huku wakijua imeghushiwa.

Inadaiwa shtaka la nne walighushi mkataba wa udhamini wa mkopo kwa wafanyakazi 11, wakawasilisha nyaraka hizo benki, walighushi tena kwa wafanyakazi 20 wakawasilisha benki na mwisho walighushi mkataba wa udhamini wa wafanyakazi 20 na kuwasilisha nyaraka za uongo Benki ya NBC.

Katika shtaka la 10 washtakiwa wote wanadaiwa kujipatia zaidi ya Shilingi bilioni nne kati ya Desemba 4, mwaka 2018 na Desemba 31, 2020 katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam kwa kutoa nyaraka za uongo Benki ya NBC Masaki wakionyesha kwamba wafanyakazi 78 waajiriwa wenye mikataba ya kudumu na Kampuni ya Peertech imewadhamini kupata mikopo.

Shtaka la 11 washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha kiasi hicho cha fedha huku wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya kughushi. Kesi hiyo itatajwa Juni nane mwaka huu, watuhumiwa wote wako rumande.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Amon Kakwale, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, pikipiki 11 zilizokamatwa katika kipindi cha Mei 15 hadi 31, mwaka huu, katika Wilaya ya Moshi, 10 kati ya hizo zikituhumiwa kupora mikoba ya kinamama nyakati za usiku na moja kusafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Majaji 3, mawakili 15 kesi vigogo CHADEMA

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Mbunge wa Mbeya Mjini (CHADEMA), Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu na mwenzake aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, wamefungua kesi ya kikatiba dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamishna wa Magereza kupinga wanachodai ukiukwaji wa haki zao wakati wakitumikia adhabu walizopewa na mahakama.

Kesi hiyo Na. 13 ya mwaka 2021 imefunguliwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ikitarajiwa kuanza kusikilizwa Juni 15, mwaka huu, ikiongozwa na jopo la majaji watatu na mawakili wa utetezi 15.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuhusiana na shauri hilo, Mchungaji Msigwa alidai yeye na viongozi wenzake walikuwa wanakabiliwa na kesi ya jinai ya mwaka 2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi.

Alisema kuwa baada ya kukamilika kwa kesi hiyo Machi 10, mwaka jana, walipatikana na hatia na kutakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 40 au kutumikia kifungo cha miezi mitano jela.

"Hatukuweza kulipa kiasi hicho kwa wakati jambo lililotufanya kutumikia kifungo jela mpaka tulipopata fedha tukalipa faini hiyo na kuachiwa huru," alisema.

Mchungaji Msigwa alisema Mbilinyi alikuwa anakabiliwa na kesi ya jinai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya na alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita bila faini.

"Mwenzangu alitumikia kifungo mpaka alipopata msamaha wa Rais Aprili 26 mwaka 2018," alisema.

Alibainisha kuwa kufungua kesi ya kikatiba kunatokana na madai ya kukiukwa kwa haki zao za kikatiba na za msingi katika kipindi ambacho walikuwa wanatumikia adhabu gerezani.

Mchungaji Msigwa alidai katika kipindi chote walichokuwa gerezani kutumikia adhabu, kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za msingi kama ilivyoainishwa kwenye katiba.

"Kitendo cha kuambiwa kuvua nguo mbele ya hadhara kwa ajili ya upekuzi wa mwili, utaratibu unaotumika ni wa kizamani na wa kinyama ambao hauzingatii umri wa mtu na faragha ya mtu, huu ni udhalilishahi wa binadamu," alisema.

Mchungaji Msigwa alidai suala la kulazimishwa kupimwa Ukimwi na kupewa majibu mbele ya hadhara na bila kufuata masharti ya kitabibu yanayohitaji vipimo kwa ridhaa na majibu kutolewa kwa siri, ni hoja yao ya pili iliyowasukuma kufungua kesi hiyo.

Alidai kitendo cha kuwafanyisha kazi wafungwa bila kuwalipa kutokana na kazi wanazozifanya nacho siyo sahihi.

"Utaratibu wa Jeshi la Magereza kuwapa wafungwa sare moja anapoingia bila kuwapa sare ya kubadili endapo imechafuka siyo sawa kwa sababu atashindwa kubadilisha," alidai.

Mchungaji Msigwa alidai kuna mambo mengi ya ukiukwaji ambayo yanafanywa dhidi ya wafungwa ikiwamo kupewa adhabu za viboko pasi na idhini ya mahakama.

Alidai kuna adhabu zinazotolewa za kumnyima mfungwa chakula ama kumpunguzia chakula, kitendo ambacho wanaona ni ukiukwaji wa haki ya kuishi.

Mchungaji Msigwa alisema kitendo cha mtu kupewa adhabu ya kutumikia kifungo gerezani haina maana ya kuondoa utu wake na kitu cha pekee anachotakiwa kukikosa ni uhuru wake na kuzuiliwa kwenda atakako.

"Tunaielekeza serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Magereza kufanya maboresho yenye lengo la kuhakikisha kwamba haki za msingi za binadamu kwa wafungwa na mahabusu zinazingatiwa wakiwa magerezani," alisema.

Mbilinyi alisema hatua hiyo ni sehemu ya uamuzi wao wa kutetea wananchi nje ya Bunge.



## SHIVYYAWATA waomba vifaa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SHIRIKISHO la Chama cha Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) mkoani Shinyanga, limeomba serikali kutenga bajeti ya kununua vifaa vya kufundishia wanafunzi wenye ulemavu.

Richard Mpongo, Mwenyekiti wa Shirikisho hilo mkoani Shinyanga, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema baadhi ya shule ambazo zinafundisha wanafunzi wenye ulemavu, wakiwamo wasioona, hazina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufundishia wanafunzi hao vikiwamo vitabu vya nukta nundu.

"Tunaiomba serikali iziangalie sana hizi shule ambazo zinatoa elimu jumuishi kwa kuwachanganya na wenye ulemavu, wahakikishe vifaa maalum vya kuwafundishia vipo vya kutosha shuleni," alisema Mpongo.

Mwalimu Josiah Nkinga anayefundisha wanafunzi wenye ulemavu katika Shule ya Sekondari Shinyanga, alisema shule hiyo inakabiliwa na vifaa duni vya kufundishia wanafunzi hao na hivyo kupata ugumu wa kufundisha.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija iliyoko Manispaa ya Shinyanga, Fatuma Jilala, alisema shule hiyo jumuishi kwa sasa haina kikwazo katika vifaa vya kufundishia wanafunzi wenye ulemavu.

Alisema kikwazo kwao kwa sasa ni upungufu wa walimu wa kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, akibainisha kuwa wanao 10 ilhali uhitaji ni walimu 18, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi wanane.




Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (wapili kulia), akikabidhi funguo ya gari dogo la mizigo aina ya Tata Ace 'kirikuu' kwa mshindi wa droo ya pili ya 'NMB Bonge la Mpango', Paulo Swai, katika tawi la NMB Tandika, mkoani Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (katikati) na Meneja wa tawi la Tandika, Ahmed Nassor (wapili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti hali ya misitu yaja

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Kituo cha Kitaifa cha Kufuatilia Kaboni (NCMC) wanatarajiwa kutoa tathmini mpya ya upotevu wa misitu nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa NCMC, Profesa Eliakimu Zahabu, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari za Mazingira (JET) alisema ripoti hiyo itatolewa kabla ya mwaka huu ili hali halisi ya misitu nchini ilijulikane.

"Tayari tumefundisha wataalamu ambao watasaidia kutupa upotevu halisi wa misitu nchini," alisema.

Alibainisha kuwa Tanzania Bara upotevu wa misitu kuanzia mwaka 2002 hadi 2013 ni hekta 469,420 kwa mwaka na Zanzibar mwaka 2004 hadi 2012 upotevu wa misitu ulikuwa hekta 3,149.

Alisema upotezaji mkubwa wa msitu ulisababishwa zaidi na kilimo cha tumbaku na kuongeza idadi ya wakimbizi ambao waliajiriwa kufanya kazi katika mashamba na wazawa.

Alisema kazi kubwa ya kituo ni kuratibu upimaji, uwasilishwaji na uhakiki wa takwimu za kaboni kwa niaba ya serikali.

"Pia kutoa huduma ya kitaalamu kwenye upimaji, uwasilishaji na uhakiki wa takwimu za kaboni kitaifa au eneo dogo ndani ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa wanasimamia viwango vya ubora wa takwimu kwenye mfumo wa kitaifa wa takwimu za kaboni.

Alisema kati ya mafanikio ya awali ya NCMC ni kuiwezesha Tanzania kutengeneza takwimu rejea za uzalishaji wa hewa ukaa itokanayo na uharibifu na upotevu wa misitu.

# Barrick yang'ara kwa mwongozo uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,**
MUSOMA

KAMPUNI ya Barrick kupitia mgodi wake wa North Mara, imetunukiwa tuzo kwa kufanikisha uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji mkoani Mara uliofanyika Viwanja vya Mwembeni mjini Musoma.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Waziri Mkuu alitumia nafasi hiyo ya kuzindua mwongozo kwa kuwakaribisha wawekezaji kuchangamkia fursa mbalimbali za uwekezaji mkoani humo na kuwahakikishia kuwa serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchi na kuondoa vikwazo vinavyozorotesha uwekezaji. Mkuu wa Mkoa wa Mara, Robert Gabriel, alishukuru wadau mbalimbali waliofanikisha maandalizi ya uzinduzi huo ikiwamo kampuni ya Barrick kupitia mgodi wake wa North Mara.

Kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo, Majaliwa alikabidhiwa tuzo na cheti kwa watendaji wa mgodi wa North Mara.

Mbali na kufanikisha uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji, Barrick imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kuboresha uchumi wa kijamii ikiwamo kukabiliana na kero mbalimbali za kijamii hususani katika sehemu zinazozunguka maeneo yake ya kazi.

Mchakato wa serikali kuanzisha mpango wa kila mkoa kuzindua mwongozi wa uwekezaji umelenga kuonyesha fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo husika, ili kuvutia wawekezaji wa nje, kukuza biashara katika mikoa hiyo na kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii. Uzinduzi huo umekuwa ukifanyika sambamba na maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali na kampuni kwa ajili ya kutangaza biashara na shughuli zao mbalimbali.

HABARI KITAIFA

## Mfumo sensa ya watu na makazi wafanyiwa majaribio

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imefanya majaribio ya mfumo utakaotumika katika sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 28, mwakani, kwa kutenga maeneo ya kuhesabia watu katika ngazi ya mtaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi, Daniel Masolwa, alisema majaribio hayo yalifanyika katika Kata ya Chang'ombe jijini hapa kama sehemu ya maandalizi ya sensa ambayo itafanyika kielektroniki tofauti na iliyofanyika mwaka 2012.

Alisema ofisi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa sensa na wajibu wa kila mwananchi katika kuhakikisha mabadiliko ya kiuchumi.

Kadhalika, alisema kundi la watu wenye ulemavu watashirikishwa kwa kiasi kikubwa kusaidia serikali katika maandalizi ya sera, tathmini na uamuzi unaotakiwa.

Masolwa alisema kuwa zoezi hilo lina hatua tatu; kwanza kuandaa maeneo ya kufanyia, kukusanya taarifa za sensa na ya tatu ni kuchambua na kutoa matokeo ya sensa.

"Kwa siku ya leo tuko hapa Chang'ombe kimajaribio kama ni hatua yetu ya kwanza kuhakiki vifaa vya kazi kama kuna upungufu kwa kuwa sensa ya mwaka huo itakuwa tofauti maana itatoa takwimu kuanzia ngazi ya chini kabisa ya kitongoji tutapata taarifa ya elimu, shughuli za kiuchumi na kama kuna mtu ana ulemavu hii itafanya serikali kujua hali halisi ya wananchi na hatua gani zichukuliwe," alisema Masolwa.

Aliwataka watakaohusika kukusanya taarifa za sensa kufanya kazi kwa usahihi na weledi ili kufanikisha lengo la serikali na itasaidia kufahamu hali halisi na uzoefu katika maeneo yote.

Alisema kuwa sensa ya mwakani watatumia vifaa vya kisasa kama vile vishikwambi (tablets), simu za mkononi na taarifa itakayokusanywa itaingia moja kwa moja katika kifaa maalumu cha kuhifadhi badala ya kutumia makaratasi.

"Vifaa hivi ni vya kisasa kwa kuwa ukifanya kosa mfumo hautakuruhusu kuingiza taarifa hadi urekebishe makosa ya awali na kabla hujafika kwenye eneo la kazi haufunguki hivyo huwezi kujaza taarifa kwa kubuni lazima ufike eneo la kazi na kila dodoso kama hujajaza kwa husahihi inagoma kuendelea hivyo umakini unahitajika," alisisitiza.

Naye Diwani wa kata hiyo, Bakari Fundikira, aliwashauri wananchi kuondokana na mtazamo hasi usio kuwa na tija kuhusu sensa ya watu itakayofanyika 2022.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe, Hadija Hamis, alisema majaribio yaliyofanyika wanatarajia kupata taarifa kamili yatakayosaidia serikali kufahamu maeneo yanayohitaji huduma au maboresho.

# SUPA Breakfast ya East Africa Radio kuja kivingine

**Na Christina Mwakangale**

KIPINDI cha redio cha SUPA Breakfast, kinachorushwa na East Africa, kinatarajia kuja na ubunifu mpya ambao utavutia wasikilizaji hususani vijana wa kisasa.

Chris Lugoe, Bobby Mongi na Evans Bukuku ni miongozi mwa watangazaji wapya ambao wataendesha kipindi hicho, kinachoanza saa tatu hadi saa nne asubuhi, siku za Jumatatu hadi Ijumaa.

Akizungumza na Nipashe mkoani Dar es Salaam, juzi, Lugoe alisema kutokana na uzoefu walio nao kwenye fani hiyo kwa takribani miaka 15, itakuwa chanzo cha kufanya kipindi kuwa bora zaidi kuliko awali.


"Umoja huu wa sisi watangazaji utafanya kipindi kuwa kizuri kuwakamata wasikilizaji zaidi hasa majira ya asubuhi ambayo kila mmoja anayesikiliza redio, atahitaji kufahamu kinachoendelea duniani," alisema Lugoe.

Naye Bobby alisema kuwa uzoefu walio nao utaleta tofauti na kwamba pamoja na kukua kwa upatikanaji habari kupitia mitandao ya kijamii, bado wasikilizaji wa redio wana fursa ya kipekee kupata taarifa zilizohakikiwa.

"Tangu kipindi kinapoanza, tayari maandalizi yamefanyika vya kutosha, pamoja na mitandao ya kijamii kutoa taarifa, lakini redio tunatoa taarifa kamili, iliyothibitishwa na zenye usahihi," alisema Bobby.

Pia Evans alisema kipindi hicho kilicho sheheni ubunifu mpya ikiwamo, burudani, taarifa za habari pamoja na mahojiano mbalimbali ndani ya studio, kitaanza Jumatatu ya wiki ijayo.

"Vipengele vipya kwenye kipindi hiki vitasaidia kudadavua 'current issues' ambazo zinatamalaki mitandaoni na sehemu zote katika vyanzo vya habari. SUPA Breakfast inamwanzishia msikilizaji siku pamoja na kumpa mwenendo wa nini kinaendelea nchini na duniani," alisema Evans. Kipindi cha SUPA Breakfast kina mchanganyiko wa matukio kadhaa, ikiwamo kufanya mazungumzo na wasikilizaji moja kwa moja, kupitia mitandao ya kijamii ya kipindi hicho na kwa njia ya simu.



Watangazaji wapya wa kipindi cha SUPA Breakfast, kitakachorushwa na EA Radio kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa tatu asubuhi (kutoka kushoto), Chris Lugoe, Evans Bukuku na Bobby Mongi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wanawake waonywa matumizi ya tumbaku

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

WANAWAKE wameshauriwa kuachana na matumizi ya bidhaa za tumbaku ili kuepuka kupata saratani ya shingo ya kizazi, kushindwa kupata ujauzito na wakati mwingine kuzaa mtoto aliyekufa.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Mkaguzi wa Dawa na Vifaa Tiba kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Dk. Yona Hebron, wakati wa kongamano la siku moja kwa wahariri na waandishi wa habari kuhusu majukumu mapya ya mamlaka hiyo.

Alisema matumizi ya tumbaku kama sigara husababisha pia mwanamke kuzaa mtoto dhaifu asiye na uzito unaotakiwa na kuwa rahisi kwake kushambuliwa na maradhi mbalimbali yanayoweza kumsababishia kifo.

Kwa upande wa wanaume, Dk. Hebron alisema bidhaa za tumbaku zimekuwa zikisababisha upungufu wa nguvu za kiume, kuharibu mbegu za kiume, kuwasababishia ugumba na kuwa na uwezekano wa kuzaa watoto watakaoshambuliwa na saratani.

Alisema nusu ya watoto wanaokufa wakiwa wachanga wazazi wao wanahusishwa kuvuta sigara kwa kuwa tumbaku huathiri mfumo wa upumuaji na kusababisha mwili wa mtoto husika kuwa dhaifu na kupata changamoto ya ukuaji wa afya yake ya akili.

Alisema sigara ina kemikali zaidi ya 4,000 na 40 kati ya hizo zimethibitishwa kusababisha saratani na zaidi ya watu milioni nane wanakufa kila mwaka kutokana na matumizi ya bidhaa zinazotokana na tumbaku.

Alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa watu saba hadi kumi wanaotumia sigara huanza kufanya hivyo wakiwa wadogo na kwamba utafiti pia unaonyesha matumizi hayo hupunguza miaka 20 ya mtu kuishi.

"Kama ulipangiwa kuishi miaka 100 kama unavuta sigara basi utaishi miaka 80, na kama ulipangiwa kuishi miaka 40 basi utaishi miaka 20 na tafiti zimeonyesha kuwa asilimia 80 ya watumiaji wa bidhaa za tumbaku wanatoka nchi maskini," alisema.

Alisema matumizi ya bidhaa za tumbaku kwenye nchi zilizoendelea yanapungua mwaka hadi mwaka wakati nchi zinazoendelea hali ikiwa tofauti kwa kuwa matumizi yamekuwa makubwa kupita kawaida.

Alisema tumbaku pia inasababisha matatizo ya ngozi, macho, pua, saratani ya mapafu na ulimi.

## Watuhumiwa 124 dawa za kulevya wakamatwa

JUMLA ya watuhumiwa 124 wa dawa za kulevya nchini, wamekamatwa katika kipindi cha Desemba 2020 hadi Mei 2021.

Pia katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2020, jumla ya dawa za viwandani (cocaine na heroin) zilizokamatwa ni kilo 426 na gramu 363.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira, Kazi na watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Malindi (CCM), Mohamed Suleiman Omar.

Mbunge huyo alihoji hatua zilizofikiwa kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

"Je, ni watu wangapi wamekamatwa kuanzia mwaka 2019-2020 na wangapi wamehukumiwa kifungo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Mhagama, alisema kati ya watuhumiwa hao 23 wametiwa hatiani na usikilizaji wa mashauri 40 unaohusisha watuhumiwa 83 unaendelea.

Pia alisema jumla ya dawa za asili (bangi na mirungi) zilizokamatwa ni tani 28 na kilo 34.

Awali, alisema katika kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini, hadi sasa serikali imechukua hatua mbalimbali.

Alitaja hatua hizo kuwa ni kutungwa kwa sheria mpya ambayo ilipitishwa na Bunge ya kudhibiti dawa za kulevya namba tano ya mwaka 2015.

"Sheria hiyo, ilianzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kama chombo maalum chenye nguvu ya kisheria ya kukamata, kupekua, kuzuia na kupeleleza makosa yote yanayohusiana na dawa za kulevya," alisema.

Alisema kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kama vile Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kitengo cha Wanamaji na Jeshi la Polisi, Serikali imeimarishaji operesheni za nchi kavu, anga na majini hasa katika viwanja vya ndege, maziwa na Bahari ya Hindi, ikiwa ni mkakati kwa kudhibiti njia na vipenyo vyote.

"Pamoja na kuendelea kutoa elimu ya athari za matumizi na biashara ya dawa za kulevya, serikali kupitia mamlaka imetambua mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya nchini na kubaini njia mbalimbali za usafirishaji," alisema.

Alisema mkakati huo, umechangia kwa kiasi kikubwa kuziba mianya ya uingizaji wa dawa za kulevya na ukamataji wa dawa hizo.

# Sheria mbalimbali kufanyiwa marekebisho

SERIKALI imesema kwasasa inaendelea kuzipitia sheria mbalimbali ikiwamo kifungu cha 131 (2) ya Sheria ya Kanuni za Adhabu ili kufanya marekebisho kutokana na uhitaji uliopo.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Rose Tweve.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kumekuwapo na mkanganyiko wa tafsiri ya umri wa miaka 18 katika sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Mtoto na Sheria ya Kanuni za Adhabu na kupelekea kuvunja misingi ya Katiba.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kuzifanyia mapitio sheria hizo husasan kifungu cha 131 (2) ya Sheria ya Kanuni za Adhabu," alihoji.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, mtu aliye na umri chini ya miaka 18 anatambulika kuwa ni mtoto.

"Pamoja na kwamba kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mtoto kinabainisha kuwa mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18, Kifungu cha 131(2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu hakitoi tafsiri ya mtoto bali kinatoa adhabu kwa mtu mwenye miaka 18 au chini ya hapo anayekuwa na hatia ya kosa la kubaka na kupewa adhabu mbalimbali.


Alisema adhabu hizo ni pamoja na kuchapwa viboko kwa mkosaji wa mara ya kwanza, miezi 12 pamoja na viboko kwa mkosaji wa mara ya pili au kifungo cha maisha kwa mkosaji wa mara ya tatu au anayerudiarudia kosa hilo.

"Kitaalamu hawa wanaitwa "young offenders" au wakosefu wenye umri mdogo," alisema.

Alisema sheria mbalimbali nje ya Sheria ya Mtoto, zinaweka umri wa mtoto kulingana na muktadha na mazingira ya jambo mahsusi kama vile mikataba, jinai, kupiga kura, leseni za udereva.

"Kufuatia kutungwa Sheria ya Mtoto mwaka 2009, iliyotokana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa 1989 pamoja na masharti ya Ibara za Haki za ujumla za Binadamu kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, na kwa kuwa Kifungu cha 131(2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kilifanyiwa marekebisho mwaka 2009 baada ya kutungwa kwa Sheria ya Mtoto, ni dhahiri kuwa hakivunji misingi ya kikatiba," alisema.

Pia alisema serikali wakati huu inapoendelea kuzipitia sheria mbalimbali, itakipitia pia kifungu hicho cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu ili kufanya marekebisho kutokana na uhitaji uliopo kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na mbunge.



Mbunge wa Viti Maalumu, Rose Tweve, akiuliza swali kwa Wizara ya Katiba na Sheria, kuhusu sheria mbalimbali ikiwamo sheria ya mtoto, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu za mfumuko wa bei nchini zatajwa

BUNGE limeelezwa kuwa mfumuko wa bei ulipanda kutoka asimilia 3.2 mwezi Desemba 2020 hadi asilimia 3.5 mwezi Januari 2021 kutokana na upungufu wa baadhi ya bidhaa sokoni.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Cecilia Paresso.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa ulioanza tangu Desemba, 2020 ambao umefanya gharama za maisha kupanda.

Akijibu swali hilo, Dk. Nchemba alisema hali hiyo hutokea mara kadhaa katika vipindi vya mwanzo mwa mwaka.

Aidha, alisema mfumuko wa bei ulishuka kufikia asilimia 3.3 mwezi Februari 2021 ikiashiria kuwa bidhaa na huduma zilianza kupatikana kwa bei nafuu kulinganisha na mwezi Januari 2021.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unaendelea kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0.

"Lengo hili linaweza kufikiwa kutokana na mikakati mbalimbali ya serikali ikiwa ni pamoja na kuimarisha usambazaji wa chakula kutoka maeneo ya uzalishaji hadi katika maeneo ya walaji, kuimarisha usimamizi wa sera za fedha na bajeti, na kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka mashambani hadi katika masoko," alisema.

Katika swali la nyongeza, alisema bei bado haijashuka sokoni hasa kwa vifaa vya ujenzi na kuhoji serikali inatoa kauli gani.

"Kwa miaka 10 sasa bado hatujapata utulivu wa bei za vyakula kama sukari, unga wa ngano, serikali inasema nini kuhusu hili," alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Nchemba alisema mfumuko wa bei ni kasi ya bei kubadilika na si bei zenyewe na kwa miaka zaidi ya 10 Tanzania imefanikiwa kushusha mfumuko huo.

"Kuna mikakati mahsusi kwenye mafuta ya kula, sukari na hotuba ya Wizara ya Viwanda ilizungumzia juu ya mkakati wa kuzalisha sukari ili kusiwe na kupanda kwa bei, uzalishaji wa ndani utatoa suluhisho la kudumu, pia kwa mafuta ya kula serikali inahamasisha juu ya mazao ya kuzalisha mafuta," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

ama

ALHAMISI JUNI 3, 2021

AFYA NA MAZINGIRA

## Utumiaji mitishamba unavyonyakua maisha ya wajawazito na watoto wao

Ukurasa 12



Ukurasa 14



## Mimba ya kidato cha 3 yamwangushia kilio bibi anayemlea mjukuu kipenzi




WIKI YA MAZINGIRA

# Darasa kuhusu namna udongo na ukanda maji unavyochafuka

Meli ikiwa majini na inatajwa kuwa inachangia uchafuzi mkubwa wa mazingira. **PICHA:MTANDAO**

Ni Wiki ya Mazingira ikiendelea. Je, kuna cha kujiuliza, Mazingira ni nini? Wataalamu wanaitafsiri kuwa ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake. Kwa hiyo, kila ulionacho ni mazingira yako.

Mazingira yanaundwa na vitu mbalimbali; yaweza kuwa ya asili kama misitu, milima, maziwa, mabonde, mito, na bahari au kutengenezwa na binadamu, kama majengo.

Shughuli za binadamu zinaweza kuwa na athari kubwa juu ya miamba ya matumbawe. Uharibifu wa misitu na uandaaji mashamba husababishwa na mmomonyoko wa mimea katika mito na maji ya pwani.

Mbolea na dawa za kuuawa kwa mazao, yanaweza kuosha au kuondokana na udongo kwenye mazingira ya maji na pwani.

Ziada ya mifugo, kuondolewa kwa mimea inaongezea mmomonyoko. Taka ya mifugo inachafua virutubisho kwenye maeneo ya pwani.

Uchimbaji unafanya kutoka kwa maji ya mvua moja kwa moja kwenda kwenye maji ya pwani. Vumbi zilizotumiwa na kutupwa au zinaweza kuharibu moja kwa moja kwa kuweka sumu mwenye maji.

Mabadiliko ya hali ya hewa, hasa katika mifumo ya mvua, mfano inaweza kuongeza mmomonyoko wa ardhi na kuharibu mchanga na uchafuzi wa maji ya pwani.

Kuongezeka idadi ya watu duniani, pia kunatajwa kuweza kusababisha ongezeko la ukubwa wa kilimo, ambacho kinaweza kuongeza matumizi ya mbolea na kukimbia.

Uchafuzi wa miamba majini, nayo inaweza kuathiri afya ya miamba. Vyombo vya kibiashara, burudani, na viwanja vya abiria vinaweza kuwa tatizo kwa miamba majini, hali kadhalika meli zinazosafiri zinachangia kwa kiasi kikubwa cha uchafuzi wa mazingira baharini.

### UCHAFUZI WA MELI

Katika wiki moja, meli ya kawaida hutajwa inazalisha mita za ujazo za 800 za majitaka; mita za ujazo 3,700 za maji; nusu mita ya ujazo ya taka; tani nane za taka imara; na karibu mita za ujazo 100 za maji ya maji machafu.

Uchafu wa baharini kutoka boti ikiwa ni pamoja na plastiki na vifaa vya kuvua vya uvuvi, navyo vyaweza kuharibu miamba.

Uvujaji wa mafuta kutoka kwa meli, nao unatajwa kusababisha kuiharibu usafi wa maji baharani na miamba yake.

Ni hali iliyoko, huku kukiwapo uvujaji mkubwa wa maji yaliyotokana na uchafu, mafuta, majitaka ghafi na taka kali katika mazingira ya baharini.

### MADHARA YA UCHAFUZI

Mosi ni usambazaji wa miti na kilimo inayoweza kusababisha mchanga, virutubisho na dawa za kupambana na dawa katika mito na hatimaye maji ya pwani.

Daraja; inavuta na kuua matumbawe na viumbe vingine na inaweza pia kupunguza uwezo wa ukuaji wa matumbawe.

Virutubisho vingi, kwa mfano, nitrojeni na fosforasi katika maji ya pwani, inasababisha kuzuia mwanga kutoka matumbawe na inaweza pia kusababisha kwa viumbe vinavyotumia oksijeni majini. Mafuta yanayotoka; husababisha uharibifu wa matumbawe na vifo, pia maji yaliyochanganyika na taka ghafi, na imara zina athari zake.

Uchafuzi wa mazingira, unaweza kushughulikiwa kupitia aina mbalimbali sera za matumizi ya ardhi, mipango na mazoea ya usimamizi katika maeneo husika.

Hizo ni pamoja na mbinu bora za kilimo zinazoweza kupunguza mmomonyoko wa mimea na kuongezeka ufanisi wa mbolea, pia hifadhi ya mazingira ya pwani, kama penye mikoko na mizinga.

### UNAVYOSHUGHULIKIWA

Uchafuzi wa maji unaweza kushughulikiwa katika namna kadhaa:

- Kuendeleza miundombinu katika bandari ili kuondoa taka zilizozalishwa kwa meli.
- Kuboresha mifumo ya kukabili majinio na kwenye meli za kusafiri na meli za mizigo.
- Njia za meli kuwa mbali na miamba.
- Kupunguza kuenea athari zinazovamia pwani.
- Kuendeleza mipango ya uharibifu mafuta yenye athari majini.

Ni muhimu kuimarisha sheria za kitaifa na kimataifa inayohusisha mikataba ya kukabili uchafuzi wa maji baharini, kwa mfano, mkataba wa kuzuia uchafuzi wa baharini na kupoteza machafu na mambo mengine 1972 au maarufu Mkataba wa London.

***Kwa mujibu wa taarifa za kisayansi***

AFYA

# Utumiaji mitishamba unavyonyakua maisha ya wajawazito na watoto wao

## •Vita vinavyowatoa jasho wataalamu afya

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MATUMIZI ya dawa za mitishamba yalikuwapo muda mrefu kihistoria ikitumika kuwa nyenzo za matibabu kutibu maradhi kama vile minyoo, kutuliza maumivu, malaria na figo.

Kwa wagonjwa kama vile wanaosumbuliwa na kifua, shinikizo la damu, degedege na homa za mapafu, kuna wengi walitibiwa kwa mitishamba iliyovunwa porini na kupatikana matokeo chanya kwa wagonjwa.

Wakati inabaki kuwa dhana inayosonga mbali ikijikita kuwa salama zaidi, pia kuna upande wa pili wa ushuhuda wa madhara na hasa kwa jamii kama za wajawazito.

Kuna dawa za tiba asili, mimea kama mwarobaini iliyotumika kutibu malaria na homa ya mapafu, dawa ya milungulungu, yote iliaminika kutibu magonjwa ya tumbo, bila ya kujua pia athari yake kudhuru ujauzito.

**MADHARA YALIVYO**

Caroline Maliseli, Mratibu wa Mama na Mtoto katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama, anasema matumizi ya dawa za miti shamba kwa wajawazito kutibu minyoo na kuongeza uchungu wakati wa kujifungua, kumechagia kusababisha vifo vyao na watoto.

Anasema, dawa hizo wazazi hutolewa zaidi na wakwe zao, wazazi hao wanatumia dawa kali kuliko mahitaji halisi na anapotumia mjamzito kuongeza uchungu, au kutibu minyoo, kunamsababisha kupasuka mfuko wa uzazi, mtoto anakunywa maji machafu na kupoteza maisha.

"Hivi karibuni tulimpokea mama mjamzito aliyekuwa amepasuka mfuko wa uzazi na mtoto amefia tumboni, baada ya kumsaidia na kumhoji zaidi alidai alipewa dawa za miti shamba za kuongeza uchungu na mama mkwe wake na ilikuwa mimba ya kwanza," anasimulia Mratibu Afya.

Anasema, wamekuwa wakitumia dawa hizo kwenye chupa ya juisi, chai na baadhi wanalamba unga wa mizizi ya dawa, huku wengine hutafuna mizizi kuongeza uchungu wa kujifungua, wengi wamekutwa nayo katika chumba cha kujifungua.

Caroline anasema, wamekuwa wakishirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali anayoyataja ya Shidepha+ na Tulonge Afya, kwa kuwatembelea wajawazito kwenye makazi yao kuwapatia elimu kuhusu dalili za hatari.



Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Regina Laurent, akiendelea kuhudumia watoto chini ya miaka mitano. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

Kinachofanyika rasmi katika hilo ni kuwapo maandalizi ya kujifungua na umuhimu wa kuhudhuria kliniki kabla na baada ya kujifungua, ili kuendelea kuangalia maendeleo ya mtoto na mama.

**MIKASA YA VIFO**

Caroline anasema, mwaka 2018 vifo vya kinamama vilikuwa 15; watoto wachanga 309; wenye umri chini ya mwaka mmoja 178; chini ya miaka mitano 236; na vizazi hai 18,360.

Mwaka uliofuata 2019 anasema, kuanzia mwezi Januari hadi Oktoba, kuna jumla ya kinamama wanane na watoto wachanga 281walikufa, wenye umri chini ya mwaka mmoja 35, waliokufa wakiwa na umri chini ya miaka mitano 189; huku vizazi hai wakiwa 16,320.

Anasema, takwimu za mwaka jana ilikuwa na vifo vya watoto waliozaliwa wafu na kufa ndani ya siku saba 266; wenye umri chini ya mwaka mmoja saba, zaidi ya mwaka mmoja 35; chini ya miaka mitano 115; na wajawazito sita nao walifariki.

Kwa mwaka huu hadi mwezi Machi, kulikuwapo na vifo vya wajawazito wawili; watoto wa umri chini ya wiki moja wako 12 na waliozaliwa wamekufa 54; wote kutoka kundi la kinamama waliojifungia ni 3,769.

**KINABABA NA KLINIKI**

Mratibu Afya anasema, hadi sasa kuna wanaume wengi kutoka katika familia duni na hawashiriki kliniki na wake zao, hali inayowafanya washindwe kuzitambua magumu au dalili mbaya zinazoweza kutokea wakati wa ujauzito, pia namna ya kukabiliana nazo.

Anasema, sehemu kubwa ya wajawazito wanahudhuria kliniki wenyewe bila ya waume, hali inayowapa mitihani watoa huduma, hasa katika hatua ya awali wakati wa kuwahudumia hasa wakati wa kupima afya ikiwamo virusi vya UKIMWI.

Vilevile anasema, kinamama wajawazito kutoka katika Halmashauri ya Msalala na Ushetu wanachelewa kuanza kliniki na hufika katika vituo vya afya kujifungua huku akiwa hana kadi ambayo inaonyesha maendeleo ya mtoto kabla ya kujifungua.

Pia anasema vituo vya afya vya Halmashauri za Msalala, Ushetu, Nzega, Tabora na Ishishimula wanachelewa, mara nyingi wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la kuchelewesha kuwahudumia wajawazito kuwaleta Hospitali ya Mji wa Kahama, wakiwa na hali mbaya.

**DED KAHAMA**

Anderson Msumba, ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, anasema katika kuondoa tatizo hilo, wameanza kujenga vituo vya afya za zahanati katika sehemu zisizokuwa na huduma hiyo, lengo ni kutokomeza vifo vinatokanavyo na uzazi.

Anasema halmashauri kwa sasa ina jumla ya vituo vya afya 22 vya serikali vinavyotoa huduma, hospitali moja, vituo vya afya vitatu na zahanati 18 na kwamba mwaka 2015. Halmashauri ilikuwa na vituo 11 vya kutolewa huduma za afya tu.

Msumba anasema, kwa sasa wameongeza vituo vya afya ambavyo kinamama wenye uzazi pingamizi wanapatiwa huduma za upasuaji wa dharura, ambazo awali ilikuwa lazima wafike katika Hospitali ya Manispaa.

Anasema wameboresha huduma za watoto wamaozaliwa wakiwa na shida au njiti, kwa kuweka huduma ya wagonjwa mahututi (ICU), yenye vifaa vya kutosha na kuwezesha kupunguza vifo vya watoto wachanga, vinavyojitokeza ndani ya siku saba au mwaka wa uzazi.

**WATUMIAJI MITISHAMBA**

Felister Benard, ni mjawazito aliyefika katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kujifungua, anasema hata yeye alikuwa anatumia mitishamba kutibu ugonjwa wa minyoo, lakini aliacha baada ya kuanza kliniki na kupewa ushauri nasaha.

Anasimulia kuwa alifundishwa kutumia dawa hizo na mama mkwe wake akiambiwa ni tiba ya minyoo na kuongeza uchungu wakati anaposhindwa kujifungua. Hata hivyo, aliziacha dawa hizo baada ya kuanza kuwa na kawaida ya kumuumiza tumbo, hata akalazimika kukimbia kituo cha afya jirani.

Naye Lucas Charles, aliyemsindikiza mkwewe kliniki anasema kuwa, suala la matumizi ya miti shamba limeanza tangu miaka ya nyuma na wao walitumia kutibu magonjwa mbalimbali, lakini hawakutumia kwa wajawazito, minyoo. wala kuongeza uchungu.

"Kipindi cha nyuma mwanamke mjamzito alikuwa haruhusiwi kula mayai, kwa sababu mtoto tumboni angekuwa na uzito mkubwa na mama kushindwa kujifungua katika njia yake. Walifanya hivyo kwa kuwa hakukuwa na vituo vya afya wala zahanati," anafafanua Charles.



Kinamama wakiwa na watoto wao wa umri chini ya miaka mitano, wakisubiri kuhudumiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

AFYA

# Sudan Kusini kunavyopoteza usalama wa madaktari, wauguzi, watoa misaada

Na Michael Eneza

MADAKTARI na wauguzi wa jumuiya ya kimataifa wanaofanya kazi nchini Sudan Kusini hasa chini ya kundi la madaktari wasio na mpaka au kifupisho chake cha Kifaransa (MSF), wanaendelea kujitafuta au kujiuliza kama waendelee kufanya kazi ya kusaidia jamii iliyo katika janga la vita, umaskini na maradhi Sudan Kusini.

Hiyo inatokana na mashambulizi ya maharamia ambayo kila mara yanalenga vituo vya afya na kama ilivyotokea hivi karibuni, hata kuua daktari ambaye ni raia wa nchi hiyo. Matukio hayo yamekuwa yakichukua sura katika maeneo tofauti; daktari aliuawa Jimbo la Kaskazini la Unity na muuguzi mwezi uliopita.

Taarifa zinasema, madaktari walitoa tahadhari ya mgomo baada ya mwenzao kuuawa Ijumaa ya Mei 21, bila ya sababu yoyote, wakati matukio ya mashambulizi yanazidi kuongezeka.

Muuguzi huyo aliuawa katika eneo la Eastern Equatoria, jimbo lililoko Kusini Mashariki mwa nchi hiyo. Umoja wa Madaktari wa Sudan Kusini (SSDU), ulielekeza kushtushwa kwake na mauaji hayo.

Unapomtaja, ukimtaja daktari aliyeuawa Louis Edward Saleh, aliyekuwa akisaidia wakazi wa kijiji cha Ganyiel katika jimbo la Unity.

Maofisa wa Umoja wa Mataifa, wanasema Sudan Kusini ni nchi hatari kwa madaktari na manesi, kwani wauguzi kutoka nje wanaofikia tisa waliuawa nchini huo mwaka jana, idadi ambayo haigusi raia wa nchi hiyo wanaofanya kazi pamoja.

Baadhi ya wafuatiliaji habari, wanasema licha ya kuwa mashambulizi katika vituo vya afya na kuua au kujeruhi madaktari na wauguzi yanastusha zaidi, kwa ujumla wafanyakazi wanaotoa misaada ya nje walioko Sudan Kusini muda wote, wako katika hatari ya kushambuliwa.

Mwezi Januari mwaka huu, mfanyakazi wa kundi la kusimamia misaada ya aina mbalimbali linaloitwa Joint Aid Management (JAM), aliuawa katika jimboni Unity, huku Shirika la Msalaba Mwekundu Duniani (IRC) likibaki kimya kuhusu kuuawa kwa Dk. Saleh, Wizara ya Afya jimboni humo inasema, uchunguzi wake umeanza.

Umoja wa Madaktari wa Sudan, walitoa tahadhari ya hali ya hatari kutokana na vitisho, kupigwa, kukamatwa na kuwekwa rumande, kuteswa na kuuawa kwa baadhi ya madaktari na wauguzi katika matukio ya kila mara.



Watumishi wa Afya wa Sudan Kusini, wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Mapema mwezi Mei, mfanyakazi wa kutoa misaada aliuawa wakati msafara wa magari ya shehena ya misaada, pale uliposhambuliwa kwa risasi Magharibi ya nchi hiyo.

Haikuelezwa ni kiasi gani cha misaada kilichoibwa au wafanyakazi wa mashirika ya misaada kunyang'anywa fedha, kwani makundi mengi ya waasi wanawalenga wafanyakazi wa mashirika ya misaada, ili wapindishe shehena ziende kwao na wazigawe.

Kimsingi, jitihada ya kimataifa ya kuwasaidia wakazi wa maeneo tofauti ya nchi hiyo ambako athari za vita ya muda mrefu tangu Sudan Kusini, imalize vita ya kujitenga na Sudan imalizike mwaka 2005.

Tangu wakati huo, watu waliokuwapo na idadi ya wanaokisiwa kufikia 380,000 wanatajwa kufa kutoka makundi ya kisiasa na kikabila yanayohasimamiana au yanayonyang'anyana ng'ombe kwa mtutu wa bunduki.

Msimamo ulioko ni kwamba, hawatambui utawala wa nchi au wa jimbo, kwamba ni kundi lililoko madarakani au lenye nguvu katika eneo husika.

Licha ya kwamba kundi kubwa zaidi la upinzani limekubali kuingia serikalini mnamo Februari mwaka jana, tayari silaha zimeshazagaa na hali ya uchumi haijatulia, hivyo wenye silaha wanatumia 'kupata mlo' kama ilivyokuwa nchini Uganda, kwa zama za Rais Idi Amin Dada.

Katika taarifa ya mwezi Aprili mwaka 2018, asasi ya jijini New York, Marekani inayofuatilia hali ya watoto katika nchi zilizogubikwa na vita, ilisema vikosi vya majeshi ya serikali na upinzani vinashambulia vituo vya afya na kudhuru kwa makusudi watendaji kazi wa mashirika tofauti yanayotia huduma.

Asasi hiyo ilisema, kulikuwapo taasisi zisizopungua 50 zilizoshambuliwa kati ya mwaka 2016 na 2017 na katika mashambulizi 750 ya wakati huo, makundi yenye silaha wakiwamo ya askari wa serikali, yalizuia misaada kufikishwa mahali mashambulizi yalikotokea.

Kwa mujibu wa mazungumzo ya madaktari na wauguzi 90 katika majimbo na Greater Upper Nile, Bahr el Ghazal na Equatoria. Christine Monaghan, mtafiti wa asasi hiyo, anasema matokeo yake ni kusambaratika huduma za afya kutokana na uharamia, askari wanaoharibu, kuchoma moto, kunyang'anya mali na kukalia kama kambi, hospitali na zahanati tofauti nchini humo. Ni balaa tupu!



AFYA

# Mimba ya kidato cha 3 yamwangushia kilio bibi anayemlea mjukuu kipenzi

## •Kapoteza mama darasa 6, sekondari hashikiki
## •Ana majibu mkato, akifunika daftari 'imetoka'



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chanzige, wilayani Kisarawe, walioshiriki mafunzo ya TEHAMA kwa vitendo, yaliyoandaliwa na Shirika la Apps and Girls likishirikiana na UNESCO wakati wa maadhimisho ya tamasha la nne liitwalo 'Africa Code Week'. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

WAZAZI wengi wanajifunga mkanda kwa kujinyima, ili walau kuwawezesha watoto wao kupata elimu itakayowakomboa kwenye lindi la umaskini.

Pamoja na juhudi hizo, wapo ambao wamejikuta katika kilio kikubwa, kwani watoto wao badala ya kuweka bidii katika masomo ili wahitimu vyema, wamekuwa wakielekeza mawazo yao kwingineko na baadhi huishia kupata mimba wangali wanafunzi, hivyo kukatisha masomo yao.

"Taarifa ya mjukuu wangu kupata mimba ililiniliza, niliwaacha walimu na kwenda kulilia kwenye mti kupunguza maumivu niliyokuwa nayo, hakika mjukuu wangu alinikumbusha maumivu ya kumpoteza mwanangu," anaeleza Zaina Msese.

Zaina, ni bibi wa binti ambaye alikatisha masomo kwa kupata mimba katika Shule ya Sekondari Chanzige mjini Kisarawe, akiwa kidato cha tatu.

Bibi huyo mwenye umri wa zaidi ya miaka 75 mkazi wa Kitongoji cha Vigama, anaeleza namna alivyohangaika na mjukuu wake kumsomesha baada ya kifo cha mama yake mzazi.

Zaina anasema, alikuwa akishirikiana na mama mdogo wa binti huyo katika malezi kumpatia mahitaji yote mjukuu ili asiingie kwenye vishawishi, lakini cha kushangaza hakusikiliza na mwisho alirudi nyumbani na mimba.

"Alikuwa akirudi nyumbani anaoga, ukimwambia soma anafunika daftari anaondoka. Ukiendelea kumzuia, anakujibu vibaya majibu ya dharau na safari zake za kutokutulia nyumbani zikaleta mimba.

"Nilianza kuona dalili, nikimuuliza kuhusiana na mabadiliko yake anasema ananenepa. Alikuwa ni mtu wa kujibu anavyotaka," anaelezea Zaina.

Zaina anasema, kilichosababisha mjukuu wake kubadilika ni makundi, pia na kutowaheshimu kwa kuwa mama yake alikuwa ameshafariki, hivyo mambo mengi alikuwa anajipangia mwenyewe.

### MKASA WA MIMBA

"Sitasahau siku niliyopata wageni walimu kutoka shuleni kwake, nililia kama mtoto. Nikikumbuka tulivyojinyima kwa ajili yake tulimfanyia kila kitu, lakini akaingia tamaa kwa kijana ambaye naye hajayajua maisha wakapeana mimba," anaeleza bibi wa binti huyo.

Zaina, sasa anaangukia rai kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa watoto wa kike waliokatisha masomo kwa kupata mimba warudishwe shuleni kuendelea na masomo .

"Ninachoomba mimi ni mjukuu wangu kuangaliwa uwezekano wa kurudi shule. Hapa alipo bado ni mdogo. Hana maarifa yoyote ya kulea mtoto zaidi ya kupata msaada na hata tukisema ataolewa umri bado mdogo, hawezi kumudu mambo ya ndoa tusaidiwe arudi tu shule," anasema.

Asma Maulid, mama mdogo wa binti huyo, anasimulia mkasa kwamba, ongezeko la mimba za utotoni katika wilaya humo inachangiwa na tamaa za wasichana.

Anaeleza kuwa binti aliyepata mimba ni mtoto wa dada yake na alikuwa akimlea yeye kwa kushirikiana na mama yake, ambaye ni bibi wa binti huyo.

"Baada ya mama yake kufariki akiwa darasa la sita, tulikuwa tukimlea kwa kila kitu alichohitaji tulimpatia, lakini haikuwa rahisi kumbadilisha tabia," anasema.

### SERIKALI MTAA

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Vigama/Sanze, Sizai Pazi, anashauri wazazi kuwasaidia watoto wa kike kusoma kwa kuwafichua wanaowapa mimba.

Sizai anasema, umbali wa kutoka shule moja ni chanzo kimojawapo cha wanafunzi wa kike kupata mimba, kwani baadhi yao wanarubuniwa wakiwa njiani kuelekea shuleni.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sanze, Catherine Thobias, anasema kuwa semina kwa watoto wa kike na wazazi kuhusiana na umuhimu wa elimu, zinatakiwa kutolewa kila mara.

Aidha, anasema wapo baadhi ya mabinti wanaopata mimba kwa kushawishiwa waache masomo na badala yake wabaki nyumbani kwa madai kuwa, hata bila ya elimu, wanaweza kuendelea na maisha mazuri.

"Mbali ya ongezeko la mimba za utotoni, pia ufaulu unashuka, kwa sababu wanaopata mimba wakijifungua wanatafuta vibarua viwandani na kufanya kazi.

"Pia, kutumia nafasi hiyo kuwashawishi waliopo shuleni kuacha kusoma ili wabaki watafute nao kazi na kupanga vyumba na kuanza kujitegemea," anaeleza Ofisa Mtendaji huyo.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Kisarawe, Patrick Gwivaha, anasema elimu inatakiwa kutolewa kwa wazazi, ili wasimamie taaluma na mwenendo wa watoto wao kwa jumla.

Gwivaha anasema, tayari wameshaanza kutoa elimu hiyo katika maeneo ya Kibuta, Masaki na Kisarawe mjini, ili wazazi waweze kuwafuatilia watoto wao kwa lengo kuinua kiwango cha ufaulu na kuondoa mimba kwao.

Anasema, kwa kipindi cha mwaka 2020 kuna jumla ya watoto 39 wa shule za sekondari wilayanio humo walikatisha masomo kutokana na mimba.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Kisarawe, Ibrahimu Msafiri, anasema uwajibikaji mdogo wa wazazi kwa watoto wao, ni chanzo kimojawapo cha ongezeko la vitendo vya ubakaji na mimba za utotoni.

Msafiri anasema, kwa kipindi cha mwaka jana, ofisi yake amepokea taarifa za matukio ya mimba kwa wanafunzi 11 wa shule za msingi na 49 wa sekondari.

Hivi karibuni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, akiwa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa, alieleza kusikitishwa na hali ya wanafunzi wanaokatisha masomo kwa kupata mimba.

Ndikilo alibainisha kuwa, jumla ya wanafunzi wa kike 130 walipata mimba katika kipindi cha mwaka 2020 kati yao, wa shule za msingi walikuwa 39 na sekondari 100.

Katika kikao hicho, alilazimika kuziomba nyumba za ibada kuingilia kati utoaji elimu kwa watoto na kuthini athari zilizoko.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alipokuwa katika kikao na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, kukithiri kwa matukio ya ubakaji katika mkoa huo, anashauri uundwaji wa madawati ya kijinsia kwenye ofisi za kata.

Anasema, ni hatua inayosaidia kuondoa tatizo hilo na mimba za utotoni kwa watoto wa kike.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, alitamka haja ya kuangaliwa utaratibu wa watoto wa kike wanaopata mimba kurudi shule kuendelea na masomo.



Mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali la 'Apps and Girls', Carolyne Ekyarisiima, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chanzige, wilayani Kisarawe, walioshiriki mafunzo ya TEHAMA kwa vitendo.



# Wamwomba Rais mchakato katiba mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameombwa kutangaza kuanza rasmi kwa mchakato wa kutungwa kwa katiba mpya kutokana na iliyopo kupitwa na wakati.

Ombi hilo lilitolewa juzi jijini hapa na wadau wa katiba na haki za binadamu katika mdahalo wa Katiba ulioandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Mmoja wa wadau hao, Deus Kibamba, alisema Katiba inayotumika sasa ina upungufu.

Alisema kutokana na upungufu huo itakuwa busara kama Rais Samia, atatangaza kuanza kwa mchakato wa kuandaa katika mpya inayoendana na wakati uliopo.

Pia alisema Rais anatakiwa kuunda tume ya wataalamu ambao watamshauri wapi sehemu sahihi ya kuanzia.

"Mchakato huu wa kupata katiba mpya umesimama sasa ni kwa takribani miaka saba na hili jambo siyo zuri sana kwani maudhui tuliyokuwa tukiyazungumzia tunaweza kuyasahau, lakini sidhani kama ni busara mchakato huu utafutwa na kuanza upya kabisa," alisema Kibamba.

Alisema katiba inayotakiwa hivi sasa ni ile ambayo itashirikisha wananchi ili kuwa na uwakilishi mpana katika kuiandaa.

"Katiba hii ya mwaka 1977, iliandaliwa na watu 20 pekee yao 10 kutoka Zanzibar na 10 wengine kutoka Tanzania Bara hivyo ipo haja kutungwa katiba mpya yenye uwakilishi mpana," alisema Kibamba.

Alisema upungufu mwingine Katiba ya mwaka 1977, ni kutungwa wakati kulikuwa na mfumo wa chama kimoja na hivi sasa ni vyama vingi na kwamba ipo kila sababu ya kupata katiba mpya.

"Katiba hii tuliyonayo naweza kusema kuwa tumerithi kutoka kwa Mwingereza na marekebisho ambayo yamewahi kufanyika ni madogo sana ambayo yana maslahi na kundi fulani na siyo kwa wananchi," alisema Kibamba.

Naye Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema ipo haja taifa kupata katiba iliyoshirikisha wananchi kutokana na iliyopo sasa kupitwa na wakati.

Alisema kutokana na Katiba hiyo kuwa ya muda mrefu haiendani na mahitaji yaliyopo hivi sasa kwa Watanzania.

"Hata katika imani yetu ya Kiislamu zamani walikuwa wanaswali mara mbili kwa siku, lakini hivi sasa tunahudhuria mara tano hivyo kuna baadhi ya mambo yanapaswa kubadilika kuendana na wakati uliopo," alisema.



Mwenyekiti wa kikundi cha Tusumuke, Christopher Dioniz (kushoto), akitoa maelezo kwa Meneja wa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Tanzania (SIDO) wa Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, namna kikundi hicho kinavyototolesha vifaranga kupitia mashine katika maonyesho ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi, Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Mtaka ataka maonyesho yenye hadhi ya makao makuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka waandaaji wa maonyesho ya kitaifa nchini ambayo yanafanyika mkoani humo kushirikisha ofisi yake ili yaendane na hadhi ya makao makuu.

Aidha, amesema ofisi yake itaanzisha kitengo cha uatamizi kwa ajili ya kulea, kuendeleza na kuzitumia bunifu mbalimbali.

Aliyasema hayo juzi katika maonyesho ya pili ya vyuo vya elimu ya ufundi yaliyoandaliwa na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), yanayofanyika jijini hapa.

Alisema mkoa huo upo tayari kuwalea na kukuza wabunifu ambao watakuwa wamebuni teknolojia mbalimbali kupitia kwenye maonyesho husika.

"Wakatitunapohitimisha maonyesho haya, Mtendaji Mkuu wa NACTE, tufanye kikao cha pamoja, nimeona hapa kuna vijana wamebuni teknolojia kwenye mita za maji, kwenye kuzuia pancha za magari wakati yanapokuwa yanatembea, kama serikali huu ubunifu tunapaswa kuulea hata kuununua," alisema.

Alisema anatarajia kukutana na viongozi wa taasisi mbalimbali zilizoshiriki maonyesho ya NACTE kwa ajili ya kufanya mazungumzo ikiwamo kupata kalenda ambazo zinaonyesha kuna matukio ya aina gani, ili kusaidia kuandaa maonyesho yenye taswira ya makao makuu.

Aliiomba NACTE kuhakikisha mwakani mkoa unakuwa ni sehemu ya maandalizi ya mashindano hayo, ili kusaidia kutangaza maonyesho hayo.

"Natarajia kukutana na taasisi zote zinazoandaa maonyesho, nahitaji kuona tunafanya nini ili tuweze kuifanya Dodoma kuonekana ni makao makuu kama ilivyo miji mingine ya nje ya Tanzania," alisema Mtaka.

Alisema anaamini kwamba maonyesho hayo na yajayo yakiboreshwa yatabadili taswira na kuchangamsha biashara ya mkoani hapo.

"Naamini tukifanya hivyo tutafika mbali na kubadilisha taswira ya maonyesho ambayo yatakuwa na tija na faida kubwa kwa wananchi na washiriki," alisema Mtaka. Aliwaomba waandishi wa habari kuhakikisha wanashirikiana na NACTE au taasisi nyingine zozote kuhakikisha wanayatangaza maonyesho hayo kwa siku zilizobaki ili jamii ijue na kujitokeza kutembelea na kujifunza. Naye Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Adolf Rutayuga, alisema mkuu huyo amekagua maonyesho katika mabanda zaidi ya 150 na kutoa ushauri vitu vya kuboresha.

## Serikali kuendelea kuwezesha wajasiriamali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa itaendelea kuwezesha wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kupata mafunzo ya kuendesha shughuli zao na kuwapatia mitaji kupitia mfuko wa kuendeleza wajasiriamali unaoratibiwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO).

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kufungua kongamano la mafundi cherehani Mkoa wa Dodoma.

Dk. Abdallah alisema, serikali ipo tayari kuwezesha wajasiriamali kufanya shughuli zao bila ya kuwapo na kikwazo chochote kwa mujibu wa sheria ili wafikie malengo yao.

"Wajasiriamali wamekuwa wakilalamika kuwa moja kati ya changamoto wanazokabiliana nazo ni pamoja na elimu ya biashara pamoja na mitaji, hili sisi kama serikali tutahakikisha tunalifanyia kazi kupitia taasisi yetu ya SIDO kwa kuendesha mafunzo pamoja na kutoa mitaji kwa kuzingitia vigezo," alisema Dk. Abdallah.

Alisema pia kupitia SIDO wataendelea kuwezesha wajasiriamali nyenzo zenye ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

"Mfuko wetu wa kuwezesha wajasiriamali una uwezo kwa kila mtu ambaye atakidhi vigezo kukopeshwa kiasi cha Shilingi milioni tano, lakini serikali kupitia Shirika la NSSF na SIDO wameingia makubaliano na Benki ya Azania ili kukopesha mtaji wajasiriamali kiasi cha Sh. milioni 50 hadi 100," alisema.

Awali, akijibu risala ya umoja wa mafundi cherehani hao, Dk. Abdallah alisema wizara yake itaendelea kuwezesha viwanda vidogo ikiwa ni sehemu ya kufikiwa kwa azma ya serikali ya viwanda.

Alisema matatizo ambayo mafundi hao wameeleza ikiwamo ukosefu wa nyenzo za kisasa watahakikisha wanafanyia kazi.

"Hivi sasa tunayo programu ya kukopesha mashine kwa ajili ya ushonaji nguo za kisasa katika Mkoa wa Mwanza, lakini na nyinyi tutaangalia wale wenye kuhitaji na kukidhi vigezo waweze kukopeshwa ili kuongeza tija katika kazi zao," alisema.

Pia alisema serikali inaendelea kuwasiliana na mamlaka husika katika maeneo mbalimbali nchini ili kupata maeneo rasmi yatakayotengwa kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli zao.

Naye mlezi wa umoja huo, Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema tayari Jiji la Dodoma limetenga ekari nane kwa ajili ya wajasiriamali.

"Tumetenga kiasi hicho cha eneo, lakini na fedha ya kuanzia kiasi cha Sh. milioni 600 kwa ajili ya kuandaa eneo hili kwa ajili ya wajasiriamali katika maeneo ya Nzunguni jijini Dodoma," alisema Mavunde.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliwataka wajasiriamali hao kuwa wabunifu katika shughuli zao za kila siku ili kulikamata soko la bidhaa zao.

"Msipokuwa makini ujio wa makao makuu ya serikali nyinyi mnaweza kuwa waangaliaji tu na fursa zote wakachukua wageni hivyo mnapaswa kuvaa sura za kazi ili mfikie malengo," alisema Mtaka.





# Kamati yaja kuchunguza mgogoro

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza kuundwa kamati maalum ya kuchunguza chanzo cha mgogoro unaofukuta kati ya mwekezaji wa mgodi wa Amos Elton uliopo kijiji cha Mlima Njiwa wilayani Chunya na mtu mwenye leseni halali ya kuchimba katika eneo hilo.

Mmiliki wa Leseni ya Mgodi huo ambaye ni Zabron Masiaga amekuwa akimlalamikia mwekezaji anayechimba madini ya dhahabu kwenye eneo hilo ambaye ni Kampuni ya Sakura Tanzania LTD kuwa anakiuka makubaliano ya mkataba huku mwekezaji naye akiwa na malalamiko yake.

Kutokana na mgogoro huo, Tume ya Madini iliamua kusitisha shughuli za uchimbaji kwenye eneo hilo mpaka wabia hao watakapofikia mwafaka na kurekebisha baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, ilifika katika kijiji hicho juzi kwa ajili ya kutatua mgogoro huo na iliposikiliza pande zote mbili ilishindwa kutoa maamuzi na ndipo ikamwelekeza Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, kuunda tume ya kuchunguza.

Kabla ya kutoa maagizo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wabia hao kila mmoja atoe maelezo ya kile kilichosababisha mgogoro huo.

Meneja wa Kampuni ya Sakura LTD, Elton Lyamuya, alisema awali wakati wanaanza kuchimba hapakuwa na tatizo lolote kati ya kampuni hiyo na mmiliki wa leseni na kwamba mgogoro ulianza baada ya uzalishaji kuanza.

Alisema mmiliki wa leseni hiyo hataki kuonana nao kwa ajili ya mazungumzo na badala yake amekuwa akiwakilishwa na Kamishna wa Tume ya Madini wa Mkoa wa kimadini wa Chunya, hali ambayo alidai inawapa wakati mgumu wa kutatua mgogoro huo.

"Mbia wetu huyu ambaye ndiye mmiliki wa leseni amekuwa akitukwepa, hataki kabisa kuonana na sisi ili tujadiliane na kufikia mwafaka, sasa hivi tumesimamisha uzalishaji ambao tulikuwa tunataka kuanza na kuna vitu tuliahidi kuwasaidia wanakijiji hatuwezi tena," alisema Lyamuya.

Kwa upande wake Shaban Werema, mwakilishi wa mmiliki wa Leseni ya Mgodi huo, alisema viongozi wa Kampuni ya Sakura Tanzania LTD wamekiuka baadhi ya makubaliano yaliyoko kwenye mkataba.

Alisema mwekezaji amekuwa akienda kuuza madini sokoni bila kumshirikisha mmiliki wa leseni kama makubaliano ya kwenye mkataba yanavyotaka na kwamba hata taarifa za mauzo haziwekwi wazi.

"Kwenye mkataba tulikubaliana kwamba mfanyakazi yeyote anayefanya kazi kwenye mgodi huu ni lazima apewe mkataba hata kama anafanya kazi siku moja, lakini tulikubaliana kwamba pande zote zinatakiwa kushiriki kwenye mauzo lakini wenzetu hawa wanakiuka," alisema Werema.

Baada ya wabia hao kujieleza, RC Homera ambaye aliiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama kwenye eneo hilo, alimwagiza iundwe kamati ya kuchunguza.

Homera aliagiza tume hiyo kuwa na wataalamu kutoka katika vyombo mbalimbali vikiwamo vyombo vya dola, Mamlaka ya Mapato (TRA), ofisi ya madini na taasisi zingine nyeti.

"Tunachotaka ni kuhakikisha mgogoro huu unafikia mwisho na uzalishaji unaendelea hapa, lakini isije ikawa kwamba mmiliki wa leseni anataka kumpatia mtu mwingine hilo hatulitaki kabisa," alisema Homera.

Aliwataka wachimbaji wote wa madini katika wilaya hiyo kuendelea kufanya kazi kwa kufuata sheria za nchi ikiwamo kulipa kodi na kuepuka kushiriki vitendo vya utoroshaji wa madini.

## Ubunifu kutatua uhaba wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa maji wameishauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), kubuni vyanzo vipya vya maji ikiwamo kuchimba visima virefu ili visaidie kupunguza tatizo la uhaba wa maji badala ya kutegemea miradi ya muda mrefu.

Katika mkutano maalum wa wadau wa maji juzi ambao ulilenga kujadili mpango wa biashara na huduma za maji kati ya mwaka 2021 na 2024, wadau hao walitoa ushauri huo.

Mmoja wa wadau hao, Sheikh Ibrahim Bombo, alisema mkoa huo una vyanzo vingi vya maji na hivyo hakuna sababu ya kuwa na upungufu wa maji, akiitaka Mbeya-WSSA, kuwa wabunifu.

Alisema katika Jiji la Mbeya kuna vyanzo vingi vya maji ambavyo bado havijatumika hivyo akasisitiza kuwa vikitumika vitasaidia kupunguza tatizo hilo la maji.

"Haiwezekani kila siku tunajisifu kwamba hili jiji letu ni 'green city' (jiji la kijani) na kila sehemu ukipita kuna viashiria vya kuwapo kwa maji lakini bado tunategemea chanzo cha Mto Kiwira kije kimalize tatizo," alisema Sheikh Bombo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole, alisema watauzingatia ushauri huo wa wadau wakati wa utekelezaji wa mipango ya mamlaka hiyo.

Alisema kwa sasa wanaendelea kusubiri utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira na kwamba mradi huo ni miongoni mwa mipango ya muda mrefu ambayo inahitaji fedha nyingi.

"Kwa sababu huu mradi utachukua muda mrefu, tunaendelea kutafuta vyanzo vingine vidogo ili kukabiliana na uhaba wa maji uliopo kwa sasa na tukimaliza ule wa Kiwira ndiyo utakuwa suluhisho la muda mrefu zaidi," alisema Mwaigomole.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Gilbert Kayange, aliwaomba wadau wa maji mkoani humo kutoa ushirikiano kwa wataalamu ili watimize majukumu yao kwa wakati na kwa ufanisi.



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya, wàkiendelea na kampeni za kumnadi mmoja wa wagombea wa nafasi ya urais wa serikali ya wanafunzi ya chuo hicho, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wanaoongoza urejeshaji mikopo elimu juu waanza kutambuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), imeanza kuwatambua waajiri wanaoongoza kwa urejeshaji wa mikopo na kuwapatia vyeti maalumu, huku ikizitaka taasisi zingine zilizowaajiri wanufaika wa mikopo hiyo kuendelea kurejesha mikopo hiyo.

Wawakilishi wa Bodi hiyo walianza kuwatambua waajiri hao kwa kuanzia katika Mkoa wa Mbeya juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Bodi ya Mikopo yaliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa HESLB, Deus Changala, alizitaja taasisi na waajiri wanaofanya vizuri kwenye urejeshaji wa mikopo kuwa ni Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Mbeya (CUcoM), Tea Company LTD, Cocacola Kwanza, SBC, HJIF, Uyole Health Center, Mbeya Cement na Shule ya Sekondari ya Panda Hill.

"Mbali na kuwatambua waajiri hawa lakini pia malengo mengine ya maonyesho haya ni kutoa elimu ya namna ya kupata mikopo kwa wanufaika watarajiwa, kutoa elimu ya urejeshaji wa mikopo pamoja na kupokea maoni ya wadau wetu," alisema Changala.

Changala ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Urejeshaji wa Mikopo Chechefu, alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa nchini yenye wanufaika wengi wanaorejesha mikopo hiyo vizuri.

Meneja wa HESLB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mtavangu, alisema katika mwaka wa masomo 2020/2021 mkoa huo una wanufaika 7,682 ambao wapo kwenye vyuo vikuu mbalimbali mkoani humo.

Alisema katika Sh. bilioni 26.7 zimekopeshwa kwa wanufaika hao na hivyo akawataka vijana waliomaliza kidato cha sita mwaka huu wanaotaka kunufaika na mikopo hiyo kufuata maelekezo wanayopewa ili wajaze fomu za maombi kwa usahihi.

"Katika Mkoa huu vyuo vimekuwa vikiongezeka kwa kasi sana, sasa hivi vipo vyuo visivyopungua nane sasa hivi, hii elimu tunayotoa lengo letu ni kuhakikisha wanaoomba wanajaza kwa usahihi," alisema Mtavangu.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya, Prof. Henry Molel, alisema katika Mwaka wa masomo 2020/2021 wanafunzi 3,734 wamesajiliwa, lakini waliopata mikopo ni 1,753 pekee sawa na asilimia 46.9.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi miongoni mwa wanafunzi waliokosa mikopo na kwamba wakati mwingine wapotoshaji wamekuwa wakijipenyeza na kuendelea kuzusha propaganda.

Aliwataka wanafunzi wanaokosa mikopo waendelee kufuatilia taarifa sahihi kutoka kwenye Bodi badala ya kusikiliza uvumi wa mitaani ambao alidai mara nyingi umekuwa ni upotoshaji.



## HABARI ZANZIBAR

# SMZ yageukia nishati mbadala

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema katika kipindi cha miaka mitano imejipanga kufanikisha uwekezaji katika sekta ya nishati mbadala.

Imesema uamuzi huo ni sehemu ya mikakati yake kuelekea uchumi wa buluu na uwekezaji wa sera ya viwanda na Zanzibar kujitosheleza katika matumizi ya umeme.

Waziri wa Maji na Nishati, Suleiman Masoud Mohamed, aliyasema hayo alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar juzi.

Alisema tayari zaidi ya kampuni nane zimejitokeza na kuonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya nishati mbadala ambayo ni miongoni mwa mahitaji ya SMZ.

Alisema wakati Zanzibar ikielekea katika uchumi wa bluu ambao ni uwekezaji katika bandari na vitega uchumi vya viwanda vya aina mbalimbali, kunahitaji kuwa na umeme wa kutosha kukidhi mahitaji na matarajio ya malengo hayo.

Alizitaja kampuni zilizojitokeza kuwekeza katika umeme wa nishati ya jua, umeme wa takataka na umeme wa upepo ni pamoja na MPS kutoka Norway.

"Malengo na mikakati ya serikali ya awamu ya nane ni kuwekeza katika umeme wa nishati mbadala kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya nishati hiyo wakati nchi ikielekea katika uchumi wa bluu kwa kuwakaribisha wawekezaji mbalimbali kuwekeza," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imejipanga kufanya utafiti wa kitaalamu kujua kiwango halisi ya maji kilichopo na matumizi yake wakati nchi ikielekea katika uwekezaji wa sekta mbalimbali muhimu za uchumi na maendeleo. Alisema utafiti huo utabainisha na kujua kiwango cha maji kilichopo katika miamba ya mawe kwa ajili ya matumizi halisi ya wananchi pamoja na sekta ya uwekezaji Zanzibar.

Mohamed alisema hayo ni miongoni mwa majukumu ambayo yanatarajiwa kutekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Salama (ZAWA) ikiwamo kuimarisha miundombinu ya maji mjini na vijijini.

Alisema serikali inatekeleza mradi wa upatikanaji maji mjini unaotekelezwa chini ya Benki ya Exim ya India ambao utamalizika mwakani na kutarajiwa kutosheleza huduma ya maji kwa wananchi.

Waziri huyo aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. bilioni 98.635 kwa ajili ya matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.Kati yake, Sh. bilioni 92.773 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Mwakilishi wa Jimbo la Kiembe Samaki, Suleiman Haroub, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Gharama kuunganisha umeme zapunguzwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamelipongeza Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja.

Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, alisema jana kuwa kitendo cha shirika kushusha gharama za kuwaunganisha wateja umeme kwa asilimia 50 kinastahili pongezi na kinaonyesha jinsi shirika hilo linavyotekeleza maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Alisema uamuzi huo kwa kiasi kikubwa sasa utawawezesha wananchi wengi kupata huduma za umeme ikiwamo vijijini na kuleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wananchi.

"Ninaupongeza kwa dhati uamuzi wa ZECO kushusha gharama za kuunganisha umeme kwa wateja kwa asilimia 50. Hayo ni mabadiliko makubwa ambayo yatasaidia kuleta maendeleo kwa wananchi wetu ikiwamo vijijini," alisifu.

Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamadi, alilipongeza shirika hilo kwa kufanikisha kufikisha umeme katika visiwa vidogo vilivyopo Pemba, hatua ambayo imebadilisha maisha ya wananchi wakiwamo wavuvi.

Alisema kitendo cha kufikisha umeme katika visiwa sita vilivyopo Pemba kimeleta mabadiliko makubwa na wavuvi wamefanikiwa kuhifadhi samaki wao katika majokofu na kuwauza kwa wakati wanaoona unafaa.

"Mimi natoa pongezi zangu za dhati kwa uongozi wa shirika la umeme kwa kufikisha nishati hiyo hadi vijijini pamoja na katika visiwa vidogo vidogo vilivyopo Pemba, hatua ambayo sisi tunaita ni mabadiliko ya kiuchumi," alisema.

Mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Yussuf Peya, aliliomba shirika la umeme kuendelea na majukumu yake ya kusambaza umeme vijijini kwa lengo la kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo na kiuchumi kwa wananchi.

Alisema katika Jimbo la Bumbwini tayari vijijini vingi vimepata huduma hiyo baada ya shirika kushusha kiwango cha kuunganisha nishati ya umeme kwa asilimia 50.

"Ninajua shirika la umeme linatekeleza mradi wa usambazaji wa umeme vijijini, ninaomba sana mradi huu uendelee kwa sababu ni muhimu katika kuyafikia malengo ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.

ZECO imepunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja kutoka Sh. 464,000 hadi kufikia Sh. 200,000 kwa eneo la mita zisizozidi 30, hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuongezeka kwa wateja na kufikia 15,605 katika kipindi cha miezi mitatu.

## Hukumu kesi ya JUMAZA Juni 7

**Na Mwandishi Wetu**

HUKUMU kesi dhidi ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) na Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar imekwama kutolewa kutokana na Jaji wa Mahakama Kuu, Rabia Hussein Muhammed, kuchelewa kuiandika.

Jaji Rabia alisema amelazimika kuahirisha hukumu ya kesi hiyo mpaka Juni 7, mwaka huu, ili kupata muda wa kuiandika kabla ya kuitolea uamuzi baada ya kukamilika kusikilizwa kwa kesi hiyo Na. 3 ya mwaka 2021.

"Hukumu ya kesi hii italazimika kutolewa Juni 7 kwa sababu bado sijaikamilisha kuiandika kabla ya kutoa uamuzi wa mwisho," alisema Jaji Rabia.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya Mahakama Kuu Zanzibar kuhusiana na uamuzi huo, Wakili wa Wadai, Oamr Shehe Omar, alisema wameridhika na uamuzi wa Jaji Rabia kusogeza mbele muda wa kusoma hukumu hiyo ili kukamilisha kuandika hukumu,

"Kwa sababu ni mara ya kwanza kuahirisha kesi ili kupata muda wa kukamilisha kuandika, hukumu upande wa wadai hatuna shaka yoyote, tunakubaliana na uamuzi wake," alisema.

Wakili huyo alisema katika hati ya msingi ya madai walalamikaji wanadai Bodi ya udhibiti wa Vileo, imevunja kifungu cha 33(1) baada ya kutoa vibali kwa kampuni za uingizaji wa vileo zaidi ya nane badala ya tatu kinyume cha Sheria Na. 9 ya Mwaka 2020.

Alidai Bodi ya Vileo inalalamikiwa kuvunja kifungu cha 28(k) kwa kuendelea kutoa leseni za baa bila ya kuzingatia masharti ya sheria kuwa kila baa kabla ya kupewa leseni, lazima iwe na umbali wa mita 1,000 kutoka maeneo ya huduma za jamii kama shule, hospitali, nyumba za ibada, makazi ya watu na madrasa, masharti ambayo hayajasimamiwa na bodi hiyo.

Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA), Shekhe Muhammed Ali Amour, alidai wamepokea bila kinyongo uamuzi wa Jaji Rabia wa kusogeza mbele muda wa kusoma hukumu wa kesi ya vileo ili kupata muda wa kukamilisha kuandika hukumu hiyo.

"Hatuna kinyongo na uamuzi uliotolewa na Jaji Rabia sababu ni mara ya kwanza kuomba muda wa kusogeza mbele," alidai.

Mwenyekiti wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar, Abdulrazak Abdulkadir, amedai walilazimika kuweka sheria kando na kuruhusu kampuni za pombe zaidi ya tatu kuingiza vileo Zanzibar kwa kulinda maslahi mapana ya mapato ya kodi ya serikali yanayotokana na vileo vinavyouzwa Zanzibar.


Sheria Na. 9 ya Vileo ya Mwaka 2020 ilianza kutumika Mei 11, mwaka jana baada ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutiwa saini na Rais wa Zanzibar, lakini imeibua mjadala mkubwa kwa makundi ya kijamii baada ya kampuni za kuingiza vileo kuruhusiwa zaidi ya nane badala ya tatu zinazoruhusiwa kisheria.

MAKALA MAALUM

# Simulizi aliyesota miaka 36 jela akisubiria kunyongwa

## ■Tangu Uhuru 1961, adhabu ya kifo imetekelezwa kwa watu 82

**Na Enock Charles**



"NIMEKAA miaka 36 jela kwa kosa la mauaji ambalo sikulitenda, nilivyotoka kwa msamaha wa rais nikakuta nyumba yangu imeuzwa kwa Sh. 400,000 na sikupewa hata shilingi moja."

Mzee Hussein Kifunza, alinusurika kunyongwa kutokana na kesi ya mauaji yaliyofanywa na anayedai kuwa alikuwa mpangaji katika nyumba yake iliyomsababishia kuhukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa mwaka 1985, lakini kilichomwokoa ni msamaha wa rais.

Alikuwa akizungumzia safari yake ya maisha na jinsi msamaha wa rais ulivyomwokoa na kutoka akiwa hai.

Anasimulia kuwa wakati huo walipohukumiwa alikuwa ni kijana wa miaka 34, akiishi Keko Magurumbasi, jijini Dar es Salaam na mpangaji wake anayedai alifanya mauaji hayo.

Akitoa simulizi hiyo kwenye chombo kimoja cha habari mtandaoni, alisema kisa cha kushtakiwa ni mpangaji wake huyo ambaye anadai alifanya mauaji jambo lililosababishwa kuja kukamatwa na polisi yeye na wenzake sita na hatimaye watatu kati yao kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa huku watatu kati yao wakiachiliwa, yeye akiwajibishwa kwa kuhusika kutokana na ushahidi wa kimazingira uliomkuta na hatia.

"Mimi wakati huo ni mwenye nyumba sasa yule rafiki yangu tuliyekuwa tunakaa naye pale alikuwa mpangaji, wakati amepanga kwenye ile nyumba nilikuwa sielewi anafanya kazi wapi ingawa aliniambia anafanya kazi kiwandani," anasimulia Mzee Kifunza.

"Siku niliyokamatwa nilishtukia tu polisi wamekuja, wakaulizia mwenye nyumba na nikajitokeza, polisi haina dogo ikabidi na mimi wanichukue."

Anasema baada ya kukamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Chang'ombe, alikuta watuhumiwa wengine wanne wakiwa wamekamatwa na jumla yake wakawa sita na kufunguliwa jalada la kesi ya mauaji la watu sita yeye akiwa mmoja wapo na akiwa ni mshtakiwa wa sita.

"Tulipofika mahakamani maeneo ya Kivukoni nikakuta pale shtaka la mauaji ya kumuua mfanyabiashara, basi ikawa kesi," anasema.

Anasema uchunguzi ulifanyika kwa miaka minne wakiwa mahabusu na mwaka wa tano ilianza kusikilizwa na baada ya miaka hiyo minne wenzao watatu waliachiwa baada ya kubainika hawakuwa na hatia na waliobaki kuhumiwa akiwamo yeye ambaye anadai alitiwa hatiani kwa kuhusika kutokana na ushahidi wa kimazingira.

"Mimi niliunganishwa kutokana na ushahidi unaoitwa wa mazingira wakati huo, hata fujo tulifanya maana aah! Tulipohukumiwa uende gerezani kwa kuny'ongwa ufe umfuate marehemu, kwa kweli roho ilibadilika sana," anasimulia.

Mwaka 2005 kipindi cha Hayati Rais Benjamini Mkapa adhabu ilibadilishwa kutoka kunyongwa hadi kufa na kuwa kifungo cha maisha na baadaye kipindi Rais wa awamu ya tano Hayati Dk. John Magufuli, wakasamehewa yeye na mwenzake mmoja huku mmoja wao akifariki kutokana na kuumwa akiwa gerezani.

Akiwa huko alisikia baadhi ya wenzao waliohukumiwa kuny'ongwa, wakiny'ongwa hadi kufa kwa awamu tofauti tofauti jambo ambalo lilimtisha na kumfadhaisha kwa kuwa hakujua na yeye zamu yake itakuwa lini.

"Mwaka 1991 nikashuhudia watu kutoka Mtwara walikuja wafungwa sita wa kuny'ongwa halafu wakaja tena watatu kutoka Tanga wakaletwa Dar es Salaam."

"Wakaingizwa kwenye gari wakapelekwa Dodoma katika waliotoka Mtwara wanne wamenyongewa Dodoma, kuna waliotoka Tanga wakanyongewa Tabora habari zilitufikia kupitia waliokuwa wamepata msamaha wakarudi huku."

"Walipofika tunawauliza vipi jamani fulani na fulani maana tunawajua majina wanatuambia wale hatupo nao walishaondoka, walishanyongwa," anasimulia.

**HABARI WENZAKE KUNYONGWA**

Anasema alipokuwa akisikia habari za wafungwa wenzao kunyongwa alipata hofu akijiua siku yoyote ingelifuata zamu yake jambo ambalo hata hivyo halikutimia.

Anasema alipokuwa huko kuna wakati walipelekwa Tanga yeye na wenzake jumla yao wakiwa 40 ili kunyongwa, lakini kitanzi kilikuwa kimeharibika na zoezi hilo kuahirishwa kwa miezi kadhaa.

Mwaka 1994 yeye na wenzake jumla yao wakiwa 30 walipelekwa mahali kwa kile alichojua kuwa ni kwa ajili ya kunyongwa na kuchukuliwa vipimo kabla ya zoezi hilo na kuingizwa katika chumba fulani chini ya ulinzi mkali wa polisi ambao anasema waliletwa hapo wakitokea katika wilaya mbalimbali za Dar es Salaam.

Anasema siku hiyo wafungwa wengine hawakufunguliwa isipokuwa waliotakiwa kunyongwa na mmojawapo ya mfungwa aliyekuwa akilala naye chumba kimoja alinyongwa huku wengine wakizimia kutokana na hofu ya kilichopo mbele yao (kunyongwa) huku kila mtu akimwangalia mwenzake kama ishara ya kuagana iwapo wengine wao watanyongwa.

Anasema siku hiyo yalisomwa majina na kwenda mahali walipowakutwa viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa wilaya, viongozi wa jela na viongozi wa dini ambao huletwa kwa ajili ya sala/swala za mwisho kabla mtu hajanyongwa yeye pia alinusirika siku hiyo.

**AKUTA NYUMBA IMEUZWA**

Pamoja na kuachiliwa kwa msamaha, mzee Kifunza anasema alikuta nyumba yake aliyokuwa anapangisha kule Keko Magurumbasi, iliuzwa kwa Sh. 400,000 za wakati huo, huku yeye akisingiziwa kupokea Sh. 200,000 jambo ambalo anadai sio la kweli kwa kuwa yeye alikuwa gerezani na hakujua kilichokuwa kinaendelea.

**MTU WA MWISHO KUNYONGWA**

Kwa mujibu wa takwimu za Amnesty International, mtu wa mwisho kunyongwa Tanzania ilikuwa mwaka 1995.

Apfili 2003, Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, alibadilisha adhabu ya kifo dhidi ya watu 100 kuwa vifungo.

Pia aliyekuwa Naibu Waziri wa Sheria na Katiba, Mathias Chikawe, aliwahi kubainisha bungeni kuwa jumla ya watu 82 walinyongwa katika awamu zote nne za serikali tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961, wakiwamo 72 katika awamu ya pili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## TANGAZO LA UKUMBI

**UKUMBI WA HARUSI NI BURE**

PR COMPLEX ILIYOPO SINZA BARABARA YA SHEKILANGO KARIBU NA HOSPITAL YA PALESTINA INATOA 'OFFER'YA UKUMBI BURE KUANZIA WATU 600 NA KUENDELEA KUNA STANDBY GENERATOR NA FULL 'AC' MAPAMBO.CHAKULA ,VITI,MEZA,MC NA MZIKI NI JUU YAKO. VINYWAJI VINAPATIKANA UKUMBINI KWA BEI NAFUU. KARIBUNI SANA.

---

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika Mahakama ya Mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi NO.133/2021
Ombi la JEILAN OTHUMAN RUBAMANGE
Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu
HAMADI RASHIDI MATENGE - BOMA ROAD

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 04/05/2021

HAKIMU

---

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika Mahakama ya Mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi NO.133/2021
Ombi la JEILAN OTHUMAN RUBAMANGE
Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu
HAMADI RASHIDI MATENGE - BOMA ROAD

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 04/05/2021

HAKIMU

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HONORY PHILIP KOBELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 543 AEE MITSUBISHI PAJERO.** CHASSIS NAMBA **CHNV360TJ00332.** ENGINE NAMBA **4M40BP4813.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/272948/2021.**

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO. 07 OF 2021
In the Matter of the Estate of the Late DAVID GWIYENH KANYATA

By OMARY DAVID KANYATA

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **21 day of 06.2021**
**Dated at MOROGORO this 2 day of 06.2021**

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO. 07 OF 2021

In the Matter of the Estate of the Late
**ORESTIS ELIAS**
By **CRISTINA CHRISTOPHER NIKITAS**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **28 day of 06.2021**

Dated at **MOROGORO** this 2 day of 06.2021
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**SUGRABAI BHAIJIBAI** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba za usajili **13928** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi (UHAMIAJI) DAR ES SALAAM mwaka 1964,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/272321/2021**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**ABDULHUSSEIN ESMAILJEE** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba za usajili **01013** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi (UHAMIAJI) DAR ES SALAAM mwaka 1933,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/272321/2021**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**ASMABAI MAMUJI ESMAILJEE** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba za usajili **09527** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi (UHAMIAJI) DAR ES SALAAM mwaka 1963,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/272321/2021**

## VYETI VIMEPOTEA



**Ndg.Samuel Michael Kitundu**

Anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo:
1) Cheti kidato cha IV chenye Index no.**S0138/0064** kilichotolewa mwaka 2012 katika shule ya sekondari-Mpwapwa
2) Cheti cha kidato cha VI chenye Index **No.S0158/0795** kilichotolewa mwaka 2015 katika shule ya sekondari Tosamaganga.

Kwa yeyote atakayekiona anaombwa aripoti kituo chochote cha polisi.
**TAARIFA YA POLISI: MBE/MBE/RB/279291**

---

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA
MAHALI MASWA
MAOMBI MADOGO NA 65 YA MWAKA 2021
ANORD K.S.TUNDUMA...................MWOMBAJI
DHIDI
MABU NGALINGA KUMILI..........MJIBU MAOMBI
WITO/TAARIFA

**Kwa: MABU NGALINGA KUMILI POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako,katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya Madai yanaweza kupatikana hapa barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa Maandishi(WSD)kabla ya tarehe 16.06.2021.
Pia unajulishwa kuwa maombi haya yanapangwa kutajwa siku ya tarehe 16.06.2021 sa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa.

Napia unafahamishwa kuwa iwapo Utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

**IMETOLEWA kwa MKONO** wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 26.05.2021

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA

---

MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA
MBEYA
SHAURI NA.27/2021
EDSON MWAIPUNGU::::::::::::::::::::::MRUFANI
Dhidi ya
MOSHA MBOKA MWANDUNGA::::::::::::::::::::::
MRUFANIWA
YAH : KUITWA SHAURINI
KWA :
MOSHA MBOKA MWANDUNGA,

Fahamu kwamba **EDSON MWAIPUNGU** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe **7/06/2021 saa 2:30** asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka :Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe **17/05/2021.**

A.Mapunda
MWENYEKITI
17/05/2021.

NAIBU MSAJILI

---

## TANGAZO LA MNADA

Kwa Idhini tuliyopewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya Tanga **TAN-GLOBAL VENTURES CO. LTD** Tutauza kwa Mnada wa hadhara nyumba iliyoorodheshwa kwenye Jedwali hapa chini ili Kutimiza Hukumu ya Mahakama

| JINA LA JUDGEMENT DEBTOR | NAMBA YA KIWANJA/KITALU | ENEO LILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| ISMAIL OMARI KASOMO | PLOT NO 3 BLOCK 40 NGAMIANI TANGA | NGAMIANI TANGA BARABARA YA 8 TANGA | 10/06/2021 |

**MASHARTI YA MNADA:**
Mnunuzi atakayeshinda atalipa 25% mara tu baada ya mnada kufungwa na atakamilisha 75% ndani ya siku 14. Fedha hiyo isipolipwa ndani ya muda mnada utarudiwa na fedha haitarudishwa .

PAUL P.KOMBA
DALALI WA MAHAKAMA - TANGA

TANGAZO HILI LIMETOLEWA
LEO TAREHE 03/06/2021
MAWASILIANO
0692693410,0714560080,0715572205

---

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM
UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
MIRATH Na. 40 YAMWAKA 2021
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ABDI NGANZI NZORI
MWOMBAJI/WAOMBAJI
KHALFANI NGANZI NZORI
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/m-wombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24th Mwezi wa June, 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 24th Mwezi wa May, 2021.

NAIBU MSAJILI

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GREENWOOD KUIKOSA EURO 2020

**LONDON, England**

FOWADI wa Manchester United, Mason Greenwood ameondolewa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England kitakachoshiriki michuano ya Euro 2020 kutokana na kuwa majeruhi.

United Jumanne walibainisha Greenwood asingekuwa kwenye kikosi cha kocha, Gareth Southgate kwa ajili ya michuano hiyo kutokana na hali yake.

Tangazo hilo lilikuja siku ambayo Southgate alikuwa akitangaza kikosi chake cha mwisho cha wachezaji 26 kutoka 33.

Katika taarifa yake rasmi kupitia kwenye tovuti United ilisema: "Mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood ameondolewa kwenye kikosi cha England kinachoshiriki Euro 2020, ili apone vizuri zaidi.

"Mason atabakia hapa Manchester United ili aweze kujiuguza tayari kwa kuanza kipindi cha maandalizi ya msimu mpya."

Greenwood alifunga mabao 12 kwenye mechi 52 katika mashindano yote kwa mashetani hao wekundu na kutoa pasi za mwisho sita msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 alitajwa kwenye kikosi cha awali cha Southgate.

# LLORIS: BENZEMA HATALETA MABADILIKO

**NICE, Ufaransa**

NAHODHA wa Ufaransa, Hugo Lloris amesema kurudi kwa Karim Benzema hakuwahakikishi mabingwa hao wa Kombe la Dunia kitu chochote kuelekea michuano ya Euro 2020.

Les Bleus hao jana Jumatano walitarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki na Wales, ambapo Ufaransa wapo kwenye kundi gumu lenye timu kama Ujerumani, Hungary na Ureno.


Fowadi wa Real Madrid, Benzema mwenye umri wa miaka 33, ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha Ufaransa baada ya miaka sita.

Nyota huyo alikuwa haitwi na kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps tangu mwaka 2015 baada ya kuhusika kwenye skendo ya kuvujisha mkanda wa ngono wa mchezaji mwenzao.

Benzema alikuwa na wakati mzuri zaidi akifunga mabao 23, 21 na 21 ya ligi kwa misimu mitatu iliyopita ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

"Kurudi kwa Karim hakubadilishi kitu chochote," alisema Lloris akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa kirafiki wa jana Jumatano dhidi ya Wales mjini Nice.

"Uwezo wake unajulikana, lakini chochote kitakachotokea kitakuja kama kawaida tu."





# ANCELOTTI RASMI KOCHA MPYA MADRID

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti ametangazwa kuwa kocha mpya wa Real Madrid akitokea Everton inayoshiriki Ligi Kuu England.

Ancelotti amechukua nafasi hiyo akiwapiku Raul na Mauricio Pochettino ambao nao walikuwa wanatajwa kuwania nafasi hiyo.

Kuteuliwa kwa kocha huyo kunamaanisha amerejea katika klabu hiyo aliyoinoa miaka sita iliyopita.

Ancelotti hakuweza kubeba taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, katika miaka yake miwili iliyopita, lakini Madrid walishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014 - likiwa la 10 katika historia ya klabu hiyo.

Madrid pia walishinda taji la Copa del Rey kwenye msimu huo na klabu bingwa ya Dunia Desemba, mwaka 2014.

Tangu alipoondoka Santiago Bernabeu, Ancelotti amezinoa Bayern Munich, Napoli na Everton, aliyojiunga nayo Desemba mwaka 2019.

Madrid ilithibitisha kuteuliwa kwa kocha huyo kupitia kwenye tovuti yake rasmi na taarifa ilisomeka: "Carlo Ancelotti ni kocha mpya wa Real Madrid, raia huyo wa Italia mwenye umri wa miaka 61 anarudi kwenye klabu hii akitokea Everton.

"Aliifundisha Real Madrid kwa misimu miwili, kati ya mwaka 2013 na 2015 na aliiongoza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atletico kule Lisbon."

Ancelotti amechukua mikoba ya Zinedine Zidane ambaye aliamua kuondoka klabu hapo baada ya msimu huu 2020-21, huku Madrid wakipoteza taji la LaLiga kwa Atletico Madrid.



# MKHITARYAN AFURAHIA KUBAKI ROMA

**ROME, Italia**

HENRIKH Mkhitaryan amebainisha namna gani alivyoangukia kwenye mapenzi na AS Roma baada ya kuongeza mkataba wake na miamba hao wa Serie A, maana yake atafanya tena kazi na Jose Mourinho.

Mkhitaryan amesaini mkataba wa kudumu wa mwaka mmoja na alikuwa akicheza mara kwa mara kikosi cha kwanza kwa msimu wa 2020-21 chini ya Kocha Paulo Fonseca.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia alifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho 11 akiwa amecheza mechi 46 kwenye mashindano yote, ikiwamo mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya timu yake ya zamani Manchester United.

Na sasa mkataba huo mpya utamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kucheza hapo kwa mwaka mmoja zaidi jijini Rome.

"Kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita hapa Roma nimeangukia kwenye mapenzi na klabu na jiji, shukrani kwa mashabiki wenye hamasa kubwa," alisema Mkhitaryan akinukuliwa na Sky Sport Italia.

Hata hivyo, Mkhitaryan sasa atakuwa chini ya Mourinho hapo kwenye dimba la Olimpico.

Mourinho alikuwa kocha wa United wakati miamba hao wa Ligi Kuu England walipomsajili Mkhitaryan kutoka Borussia Dortmund Julai, mwaka 2016.

Kiungo huyo kwa kipindi hicho alicheza kwa mechi 41 katika msimu wake wa kwanza hapo Old Trafford, lakini hakuweza kupata nafasi msimu uliofuata baada ya kukosa nafasi chini ya Mourinho.

Na baadaye akajiunga na Arsenal Januari mwaka 2018 katika dili lililomhusisha Alexis Sanchez kwenda upande mwingine.

## SUAREZ SASA ALITAKA TAJI LA UEFA

**MADRID, Hispania**

LUIS Suarez amesema anatamani kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Atletico Madrid.

Nyota huyo kwa sasa yupo katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Uruguay inayojiandaa na michuano ya Copa America.

Suarez alishinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, akiwa na Atletico Madrid baada ya kutemwa kule Barcelona msimu uliopita.

Lakini sasa akitazama mbele kwa siku zijazo anaona kwamba, ni wakati wake sasa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Atletico.

"Nina njaa na taji hili," alisema Suarez katika mahojiano na Ibai Llanos.

"Kila wakati unapomaliza msimu, unafurahia jinsi ilivyomaliza, lakini tunataka kuanza tena.

"Nitazingatia timu ya kitaifa kwa sasa, lakini baadaye Atletico.

"Niliiambia klabu kuwa sina shida na kwamba mimi na familia yangu tunafurahi kukaa.

"Kila wakati ninapofikiria juu ya msimu mpya, kuna changamoto mpya na matumaini na hii ndivyo nitakavyokuwa siku zote, nikitaka kushinda.

"Si lazima ukate tamaa, kwa nini usifikirie juu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya? Itakuwa

# STERLING, JESUS CHAMBO KWA KANE

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City wameripotiwa kuwa tayari kumtoa Raheem Sterling na Gabriel Jesus kwa Tottenham Hotspur kwa ajili ya kumnasa mshambuliaji nyota, Harry Kane.

Baada ya kuchapwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Chelsea, City wanahusishwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa England msimu huu wa joto wakati wanaimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Spurs wanasita kumuuza mchezaji huyu akiwa amebakiza miaka mitatu kwenye mkataba wake, haswa kumuuza kwa hasimu wao wa moja kwa moja wa Ligi Kuu England.

Kwa mujibu wa The Sun, City wanaamini kwamba wanaweza kuwashawishi Tottenham kufanya biashara kwa kutoa washambuliaji kadhaa ili kumpata Kane.

Hata kama Spurs wangependa kumsaini Sterling na Jesus, City bado italazimika kulipa fedha nyingi.

Jesus alifunga mabao tisa na kutoa usaidizi kwenye mengine manne katika Ligi Kuu msimu wa 2020-21, wakati Sterling alihusika moja kwa moja katika mabao 17.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AKUBALI KUSAINI MIAKA MIWILI BARCELONA

●●● Uamuzi huo unazifanya tetesi za kuondoka klabuni hapo kuzimika rasmi huku akiungana na...

**BARCELONA,** Hispania

MSHINDI mara sita wa tuzo ya Ballon d'Or, Lionel Messi anapanga kusaini mkataba mpya wa miaka miwili wa kuendelea kuitumikia Barcelona, kwa mujibu wa AS.

Uvumi wa majaliwa ya Messi umekuwa mjadala mkubwa zaidi katika miezi ya hivi karibuni, huku akielekea kuwa mchezaji huru mwisho wa mwezi huu.

Messi kabla ya kuanza kwa msimu huu aliomba kuondoka Katalunya kabla ya baadaye kukubali kuendelea kucheza kwa msimu mmoja zaidi.

Barca tayari wamemsajili Sergio Aguero na Eric Garcia kutoka Manchester City kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu ujao.

Ujio wa Aguero ambaye ni rafiki wa Messi tangu utotoni unaonekana kumshawishi mshambuliaji huyo nyota kubakia klabuni hapo kwa misimu mingine.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania, Messi amekubali kusaini mkataba wa miaka miwili kuendelea kubakia kucheza hapo.

Awali Messi alikuwa anataka kwanza kuhakikisha kujengwa kwa kikosi hicho ili akukubali kuongeza muda wa kucheza hapo.

Kabla ya Messi kukubali kusaini mkataba mpya, alikuwa akitajwa anawaniwa na klabu kubwa Ulaya kwa kiasi kikubwa cha fedha.

Timu kama Manchester City na Paris Saint-Germain zote zilikuwa zinahusishwa sana na usajili wa Messi, lakini sasa anaonekana kukubali kuongeza mkataba hadi mwaka 2023.

## KWA UFUPI

### BENITEZ ANUKIA EVERTON

EVERTON watafikiria uwezekano wa Kocha wa Rangers, Steven Gerrard na kocha wa zamani wa Liverpool, Rafael Benitez kuchukua nafasi ya Carlo Ancelotti. (***Athletic***)

### NUNO AINGIA SOKONI

KOCHA wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo naye yuko kwenye orodha ya makocha wanaotakiwa na Everton kuelekea katika maandalizi ya msimu mpya. (***Talksport***)

### BENITEZ APIGIWA DEBE

NYOTA wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher anaamini kuwa kocha wa zamani wa klabu hiyo, Rafa Benitez ni chaguo bora kuchukua nafasi hiyo kule Everton. (***Telegraph***)

### STERLING ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wanaongoza kwenye mbio za kumsajili winga wa Manchester City, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26.(***Sun***)

### UNITED, BARCA VITANI

MANCHESTER United wanakabiliwa na ushindani katika kumnasa mlinzi wa Sevilla, Jules Kounde kwani Barcelona pia ina mpango wa kumsajili mchezaji huyo raia wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22. (***Mundo Deportivo***)

### ONANA AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL wanajiandaa kukamilisha taratibu za kumsajili mlinda mlango wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, kutoka Ajax, kwa ada ya pauni milioni 1.7 (***Nos-in***)

### ABRAMOVICH AMTAKA LUKAKU

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich ana mpango binafsi wa kumchukua mshambuliaji wa Ubelgiji anayekipiga Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28. (***Eurosport***)

### TUCHEL APEWA NGUVU

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel atapatiwa mpaka pauni milioni 200 kwa ajili ya usajili katika kipindi hiki cha majira ya joto. (***Metro***)

### PJANIC KUREJEA JUVE


KIUNGO wa kati wa Barcelona, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31, anataka kurejea Juventus. (***Tuttosport***)

### DONNARUMMA AWINDWA

KOCHA mpya wa AS Roma, Jose Mourinho anawaniwa kumsajili golikipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 22. (***Mirror***)

### UNITED YAMTAKA PEDRO

MANCHESTER United wanamtolea macho kiungo wa kati wa Sporting Lisbon, Pedro Goncalves mwenye umri wa miaka 22. (***Record-via Star***)



HABARI MICHEZO

# WABONGO WAMPONZA SAMATTA KUREJEA VILLA

Na Adam Fungamwango

MANENO ya baadhi ya Watanzania katika akaunti za mitandao ya kijamii ya Aston Villa yakamponza nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta kurejea katika klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England baada ya kumaliza mkataba wake wa mkopo nchini Uturuki.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Samatta ambaye mkataba wake wa mwaka mmoja wa mkopo na Fenerbahce ya Uturuki unamalizika, ameonyesha wasiwasi kama anaweza kudumu sana Aston Villa kutokana na maneno ambayo Watanzania waliyaandika wakati anaondoka kuelekea Uturuki.

"Watanzania baada ya kuondoka Aston Villa waliongea maneno makali sana, kwa hiyo sijui kama nikirudi nitakaribishwa au nitafukuzwa. Nadhani nitarudi lakini sijui kama nitakaa kwa sababu Watanzania bwana, wengi waliongea maneno makali sana, sasa huwezi jua kama watakuwa wamenikasirikia," alisema Samatta.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), aliondoka Aston Villa mwanzo mwa msimu huu baada ya kuichezea timu hiyo ya Ligi Kuu England kwa miezi sita tu, huku akiwa amesaini mkataba wa miaka minne na nusu.

**Nyota huyo wa zamani wa African Lyon, alijiunga na Aston Villa, Januari mwaka 2020 aki tokea KRC Genk ya Ubelgiji.**

Baada ya kujiunga, Watanzania wengi waliingia katika akaunti za mitandao rasmi ya kijamii ya Aston Villa na kuandika ujumbe wa kuishabikia timu hiyo, lakini baadaye waligeuka na kuwa mwiba kufuatia kutangazwa nyota huyo anatolewa mkopo.

Baadhi ya maneno ya mashabiki hao yalilenga kuonekana mchezaji huyo ananyimwa ushirikiano na wachezaji wenzake kama vile kupewa pasi akiwa kwenye nafasi ya kufunga, hivyo kuwanyooshea vidole baadhi ya wachezaji wa timu hiyo.

Hali hiyo ilileta mkanganyiko hadi Samatta mwenyewe alilazimika kuandika ujumbe wa kuwatuliza mashabiki wake kwa kuwasihi waache tabia ya kuwashutumu wachezaji wenzake, kitu ambacho pia kilipingwa na mashabiki hao, wakimtaka acheze soka, kazi ya mitandao ya kijamii awaachie wao.

Hata alipoondoka kwenda Fenerbahce, baadhi ya Watanzania waliandika maneno makali, ikiwamo wengine kujiondoa kwenye ukurasa wa mtandao wa klabu hiyo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, ACP Ramadhan Kingai (katikati), akipokea mipira kutoka kwa Mwakilishi wa Kampuni ya Silent Ocean, Mohamed Kamilagwa (kulia), kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya majeshi. Kushoto ni Mkuu wa Michezo wa Jeshi la Polisi, ACP Jonas Mahanga. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jeshi la Polisi lapewa vifaa

Na Sabato Kasika

JESHI la Polisi limepata msaada wa vifaa mbalimbali vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 11.5 kwa ajili ya kutumika katika mashindano ya majeshi inayotarajiwa kufanyika kuanzia Juni 10, mwaka huu jijini Dodoma.

Baadhi ya vifaa hivyo ni jezi, mipira, soksi, viatu, ambavyo vimetolewa na Kampuni ya Silent Ocean na kukabidhiwa kwa Kamanda ya Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, ACP Ramadhan Kingai.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, Kamanda Kingai, alisema mashindano hayo yatashirikisha Jeshi la Wananchi, Polisi, JKT, Magereza, Zimamoto na vikosi vya kanda kutoka Zanzibar.

Sirro alishukuru kupata msaada huo wa vifaa vya michezo kwa sababu utaongeza unyonge wa kutokuwa navyo na utaongeza ari ya mazoezi kwa wanamichezo wa vikosi vyote wanaoendelea na mazoezi.

Mkuu wa Michezo wa Jeshi la Polisi, ACP Jonas Mahanga, alisema mashindano hayo yanalenga kukuza uhusiano katika vyombo vya ulinzi na usalama nchini na yamekuwa yakifanyika kila mwaka.

"Mwaka jana hatukufanya kutokana na ugonjwa wa corona, lakini sasa hali imetulia ndio maana wanamichezo wetu wako kambini wakiendelea kujifua kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo," alisema ACP Mahanga.

Mwakilishi wa Silent Ocean, Mohamed Kamilagwa, alisema majeshi mengi yalikuwa yameomba vifaa vya michezo, lakini muda ukawa mchache wakaamua kuanza na Jeshi la Polisi.

## Bocco, Manula waiamsha Azam

Na Saada Akida

BAADA ya kumwongeza mkataba mpya mshambuliaji wake tegemeo kutoka Zimbabwe, Prince Dube, uongozi wa Azam FC umesema haukua tayari kurudia makosa waliyoyafanya misimu mitatu iliyopita kwa muuza Kipre Tchetche huku wakiwa hawana mchezaji mwingine mbadala.

Dube amesaini mkataba miaka miwili kuendelea kuitumikia timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin `Popat` alisema hawafikirii kumuuza Dube na hata mchezaji yeyote yule ambaye yuko katika mipango ya kocha wao, George Lwandamina.

Popat alisema hatuwezi kurudia makosa ya nyuma ambayo walimuuza Kipre Tcheche ilhali hawakupata mbadala wake na kushindwa kufikia malengo ambayo wamejiwekea ikiwamo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara na kukata tiketi ya kushiriki michuano ya Kimataifa.

"Kwa msimu huu hatuuzi mchezaji labda msimu ujao, maana tukirudi nyuma tunakumbuka jinsi tulivyoyumba kipindi tulichomuuza Kipre bila ya kuwa na mbadala wake na kushindwa kufanya vizuri, sasa hatutakubali litokee kwa Dube".

"Tuna jicho moja halafu hilo hilo tulitoe, hatutakubali kwa sababu sasa mipango yetu ni kujenga timu imara kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu kwa ajili ya msimu ujao," alisema Popat.

Aliongeza wataendelea kufuata mapendekezo ya Lwandamina kwa kuhakikisha wanawabakisha wachezaji wanaokaribia kumaliza mikataba yao ili wasije kuondoka kama ilivyotokea kwa John Bocco, Aishi Manula na Erasto Nyoni ambao sasa wanang'ara katika kikosi cha Simba.

## Hard Rock FC yashuka daraja

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Hard Rock yenye makazi yake Kisiwani Pemba imeshuka daraja kutoka Ligi Kuu Zanzibar msimu huu baada ya kupokea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa JKU katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi.

Kwa matokeo hayo Hard Rock imeendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi 19 ambazo hata ikishinda mchezo wake mmoja uliobakia haiwezi kunusurika na janga hilo.


Wakati huo huo waliokuwa mabingwa watetezi, Mlandege imeondoka katika mstari wa hatari wa kushuka daraja baada ya hapo kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi na kufikisha pointi 25 huku mkononi akibakisha mchezo mmoja dhidi ya Malindi.

Mlandege ili kujihakikishia kutoshuka daraja msimu huu anatakiwa ashinde mchezo wake huo wa mwisho ambao utamfanya afikishe alama 28.

Polisi yenye pointi 24 nayo imeendelea kuwa tumbo joto baada ya kupoteza mchezo wake dhidi ya Mlandege hapo juzi na ili kubakia kwenye ligi hiyo ya juu inahitaji kumwombea dya mbaya Chuoni yenye alama 23 afungwe mchezo mmoja kati ya miwili iliyobakia huku pia akindisha mchezo wake wa mwisho dhidi ya KVZ.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea leo kwa mabingwa wapya KMKM kuwaalika Chuoni huku KVZ wakivaana na Mafunzo.

Michezo
Alhamisi Juni 3, 2021
Nipashe



MESSI AKUBALI KUSAINI MIAKA MIWILI BARCELONA HABARI UK 22

# SIMBA YAITANGAZIA VITA RUVU SHOOTING

●●●Lengo ni kuendelea kuusogelea ubingwa huku Maafande hao wakitamba sasa...

**Adam Fungamwango na Richard Makore, MWANZA**

MBIO za kuwania ufalme wa soka Tanzania zinatarajia kuendelea kwa vinara na mabingwa watetezi, Simba kuvaana na wenyeji Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza jijini hapa jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema kikosi chao kipo vizuri na tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wamejipanga kuondoka na ushindi ili kujiimarisha kwenye mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Matola alisema wachezaji wote wako vizuri na wanafahamu mechi hiyo haitakuwa nyepesi kutokana na historia na timu hizo mbili zinapokutana.

Alisema nia yao ni kupambana na kuondoka na pointi tatu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuchukua ubingwa na kuwataka wachezaji, Joash Onyango na kiungo, Clatous Chama ni nyota watakaokosekana katika mechi ya leo.

"Tumefanya maandalizi vizuri, sio mechi rahisi, ni mechi ngumu kwa sababu katika mechi ya kwanza Ruvu walitufunga katika mechi ya nyumbani, huwezi kupata ubingwa kama huwezi kuchukua pointi tatu katika kila mechi iliyoko mbele yako, nia yetu sisi ni kutetea ubingwa," alisema Matola.

Nahodha Msaidizi, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema wamesahau matokeo ya mechi iliyopita na katika mchezo wa leo wataingia wakiwa na nguvu mpya.

Naye Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting, Rajabu Mohammed, alisema wamejipanga kuhakikisha wanapambana ili wapate ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo itateremsha timu nne moja kwa moja.

Kocha huyo alitamba timu yake itaibuka na ushindi mnono katika mchezo huo kwa sababu wana kikosi kizuri ambacho kimeandaliwa vyema kuondoka na pointi zote tatu.

Msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire alitamba wamejipanga 'kumtafuna' Simba kwa mara nyingine lakini safari hii ikiwa ni kwenye eneo la tumbo.

"Sisi leo tutamla simba husisan eneo la tumbo, hatutaki kichwa kwa sababu huwa kina mambo mengi, hatuna namna nyingine ya kufanya, tunajua Simba wanafikiria kuja kulipiza kisasi. Hilo wasahau kwani sisi tupo tayari kuwafunga kwa mara nyingine tena na kudhihirisha sisi ni zaidi yao," Bwire alisema.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Oktoba 26, mwaka jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Simba ilichapwa bao 1-0 mbele ya aliyekuwa kocha wao mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Simba itashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake tano za mwisho za Ligi Kuu, ikianza kwa kuichapa Mtibwa Sugar mabao 5-0, ikaifunga Mwadui bao 1-0, ikaisasambua Kagera Sugar mabao 2-0, ikaidungua Gwambina goli 1-0 na kuiadhibu Namungo mabao 3-1.

Baada ya mechi ya leo, ligi hiyo itasimama kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa kuwakaribisha Malawi katika mechi ya kirafiki itakayochezwa Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.



Winga wa kimataifa wa Simba kutoka Ghana, Bernard Morrison (kushoto), akiwania mpira dhidi ya kiungo wa timu hiyo, Hassan Dilunga katika maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. **PICHA: SIMBA SC**

## NABI AFUNGUKA NJIA YA UBINGWA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema bila ya kusimamia nidhamu kwa wachezaji wake, kamwe kikosi hicho hakiwezi kufanya vizuri katika michezo yake iliyobakia na kufikia malengo waliyojiwekea katika msimu huu wa mwaka 2020/21 ambao unaelekea ukingoni.

Yanga imebakia mechi tano za Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ikiwa pia imetinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake hukata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shikisho Afrika.

Nabi aliliambia gazeti hili anaendelea na jitihada za kutengeneza kikosi imara ili kufikia malengo ya klabu, lakini akaweka wazi hawezi kupata mafanikio kama suala la nidhamu ya wachezaji wake halitazingatiwa.

Kocha huyo alisema kamwe malengo hayawezi kutimia kama hakutakuwa na nidhamu, na kuongeza endapo kila mchezaji atazingatia jambo hilo, ana imani kwa uwezo waliokuwa nao nyota wake, watamaliza msimu kwa furaha.

"Nyota waliokutana na adhabu ni mfano kwa wengine ambao wana tabia za kujiona wakubwa kuliko klabu, tangu nimekuja hapa nimekuwa nikifuatilia mienendo ya wachezaji wangu, nataka kujenga kikosi imara kitakachoogopeka Afrika, nitafanikiwa katika hilo iwapo suala la nidhamu itakuwa vizuri, nina uhakika nitasimamia hili bila kuangalia kiwango cha mtu," alisema Nabi.

Aliongeza mchezaji atakayefuata matakwa ya klabu wataendelea kuwa naye kikosini na yule ambaye atashindwa kuendana na kasi, ameacha milango wazi kwa sababu bado malengo yao ni kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na kutwaa ubingwa wa Kombe la FA.

Alisema pia nidhamu ya wachezaji ni silaha kubwa ya kupata mafanikio ambayo yanayotarajiwa ikiwamo suala la kufanya vizuri katika michezo iliyobakia itafikiwa.



Yanga yenye pointi 61 baada ya kucheza mechi 29 za Ligi Kuu Tanzania Bara, imebakiza michezo mitano, lakini itacheza mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Biashara United kati ya Juni 24 na 27, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042